

Wabunge waliofukuzwa wapasua Chadema **Uk. 20**



Bashe

Mpina ameanza safari au anafika mwisho?



Mpina

Soma Uk. 12

Sumaye: Rais Magufuli nusura azamishe nchi **Uk. 4**



Waziri Mkuu Mstaafu, Frederick Sumaye, akizungumza na Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Pambazuko, Peter Nyanje (kushoto) na Mwandishi Mkuu, Elizabeth Hombo wakati wa mahojiano maalum na gazeti hili ofisini kwake jijini Dar es Salaam juzi. (Picha na Fidelis FELIX)

Atamani Mwalimu Nyerere aamke kumtandika Dkt Dimwa

Soma zaidi Uk. 5

Ndani

Safu kamambe

- Askofu Bagonza
- Dkt. Kijo Bisimba
- Evarist Chahali
- Jicho la Tai

Mnada Pugu wageuzwa shamba la bibi

- Kuna ufisadi wa kutisha
- Vigogo wizarani wamo

soma Uk. 6

Tahariri/Katuni

Kodi: Serikali sikivu ni haki, siyo ubabe

WATANZANIA bado wana kumbukumbu za kauli za kibabe na kiburi cha dhamana na uhai, zilizowahi kutolewa na “wakubwa” wetu kwa nyakati tofauti.

Kauli hizo zilibeba na zinaendelea kuonyesha kuwa – kwa Katiba ya sasa ya Tanzania, rais na serikali anayoiongoza, wanaweza kuamua lolote, ili muradi wanayotaka yawe, yanakuwa, bila kujali maumivu yake kwa watu wanaoongoza.

Moja ya kumbukumbu mbaya inayoendelea kuishi hata leo, ni kauli aliyowahi kuitamka Basil Mramba, wakati huo akiwa waziri wa fedha.

Mramba alisema kwamba “Watanzania tutakula hata nasi, lakini ndege ya kurahisisha safari za rais, lazima inunuliwe. Kauli hii ilifuatia kelele za wananchi kupinga serikali kununua ndege “ya bei aghali” kwa safari za rais.

Kweli, pamoja na kelele hizo, serikali wala rais wa wakati huo – Benjamin Mkapa hawakusikiliza, ndege ikanunuliwa na “kelele zikaisha.”

Mbali na kauli hiyo ya kibabe, waziri wetu wa fedha wa sasa, Mwigulu Nchemba naye aliwahi kusikika akitamka kuwa tozo kwa matumizi ya simu za mkononi, lazima ziongewe – watu

watake wasitake, na kwamba asiyependa tozo hizo, “ahamie Burundi.”

Kauli hii ya Mwigulu ilileta tafrani maeneo mengi ya nchi yetu na hasira za wananchi zilionekana kupitia vyombo vya habari kulaani kauli hiyo. Hata hivyo, tozo ziliongezwa na kelele zikaisha.

Hivi karibuni, serikali kupitia kwa Mwigulu, ilipeleka matamanio yake kuongeza kodi kwenye gesi asilia inayotumika kuendeshea magari.

Kodi hiyo ilipigiwa kelele nyingi kupinga na gazeti hili likiwa mstari wa mbele kukataa na kuishauri serikali kuiondoa.


Katika Bajeti Kuu ya Serikali aliyoisoma bungeni hivi karibuni, Mwigulu, alionyesha ukomavu wa kusikiliza wananchi, kiasi kwamba serikali iliamua kuondoa kusudio lake.

Ileweke kuwa tabia ya usikivu kwa serikali, ndiyo hasa Watanzania wanapenda kuona viongozi wao wakiitukuza na siyo ubabe.

Pambazuko, kama ilivyo kwa wananchi wengi, linaamini kuwa kamwe ubabe haujengi, isipokuwa kudunduliza chuki ambayo mwisho wake, hauna tija kwa maendeleo ya Tanzania.



Jeshi la Kenya Haiti...



Komandoo wa Jeshi la Kenya akilinda ubalozi wa Marekani huko Tabarre, Haiti kama alivyonaswa na kamera ya Patrice Noel. Wakenya wengi wamekuwa wakipinga hatua ya Rais William Ruto kuruhusu jeshi la nchi hiyo kutumika Haiti.

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mhariri wa Habari	:	Maregesi PAUL	0689 732 325
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz



Sumaye: Magufuli nusura azamishe nchi



Waziri Mkuu Mstaafu, Frederick Sumaye, akizungumza na Pambazuko wakati wa mahojiano maalum na gazeti hili ofisini kwake jijini Dar es Salaam juzi. (Picha na Fidelis FELIX)

Na Elizabeth HOMBO

UTAWALA wa John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano wa Tanzania, ulikuwa unaiingiza nchi kwenye tanuri la maangamizi.

Kwamba Tanzania ilikuwa inakaribia kupoteza sifa yake kubwa ya kuwa nchi ya kupigiwa mfano katika maeneo mengi; ikiwamo amani, umoja, mshikamano na utulivu, kwani Rais Magufuli hakuwa muumini wa tunu hizi.

Haya ni mawazo, mtazamo na maono ya Waziri Mkuu (mstaafu), Frederick Tluway Sumaye (74) aliyoyaweka wazi kwa umma wakati akihojiwa na gazeti la Pambazuko, jijini Dar es Salaam, juzi – Jumamosi.

Kutokana na mtazamo wake kuhusu “staili” ya utawala wa Magufuli, Sumaye anasema; “utawala wa awamu ya tano chini ya Rais Magufuli, ulikuwa unaizamisha nchi.”

Sumaye ambaye ndiye waziri mkuu pekee aliyetumikia nchi kwa kipindi kirefu cha miaka kumi katika serikali ya awamu ya tatu – chini ya Rais Benjamin William Mkapa, amesema lakini hivi sasa Rais Samia Suluhu Hassan ameirudisha nchi mahali pazuri na sasa iko salama.

“Awamu ya tano iliifikisha nchi mahali am-

bapo ilikuwa inakaribia kuzama, lakini sasa matumaini ya Watanzania yaliyokuwa yamepotea, yameanza kurejea kutokana na anayoyafanya Rais Samia,” alisema Sumaye katika mahojiano maalumu na waandishi wa gazeti la Pambazuko yaliyofanyika ofisini kwake Mwananyamala.

Pamoja na mambo mengine Sumaye alizungumzia utawala wa Rais Samia akiulinganisha na ule wa Dk. Magufuli.

“To be frank (maneno ya Kiingereza, yenye maana kwamba – “naomba kuwa mkweli”) mama Samia... mimi kwanza ninampenda, kwa hiyo unajua anaendesha nchi bila makeke, lakini pia amerudisha matumaini ya Watanzania yaliyokuwa yamepotea,” amesema.

Mwanasiasa huyo mkongwe ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Hanan’g kwa miaka 22; kuanzia mwaka 1983 hadi 2005, alieleza kushangazwa kwake kwa baadhi ya watu wakati wa utawala wa Rais Magufuli waliokuwa wanasema anaipoleka nchi pazuri lakini “wenye akili waliokuwa wanaona nchi inazama...”

“Unajua watu hawaelewi. Uelewa wa Watanzania ni tofauti sana. Kuna watu walikuwa wanaona na wanasema Rais Magufuli alikuwa anaipoleka nchi kunakotakiwa, lakini wenye akili zao walikuwa wanaona nchi inazama kabisa...”

“Mimi nilikuwa najua nchi inazama na ilikuwa imeshafika mwisho kabisa, angalau mama Samia ameirudisha katikati kwenye usalama, sasa katika hilo kwa kweli mimi nina matumaini makubwa...”

“Kila mtu ana matatizo yake, hakuna aliyekamilika hapa na pale, najua wanamsema Rais Samia kwa hili na lile, lakini mimi nasema ‘generally’ (kwa ujumla) kama nchi ukiangalia anakoiipelekea ni salama...”

“Sasa ‘speed’ (kasi) ya kwenda inategemea na mambo mengi, lakini angalau direction (mwelekeo) unauona. Leo hakuna mfanyabiashara ambaye anaogopa kufanya biashara kwa sababu mali yake itanyang’anywa, watu wa kodi wanafanya vituko hapa na pale, lakini nao

Atamani Nyerere aamke kumtandika Dimwa

Na Igo Al

RAIA mmoja wa makamo, anayekadiriwa kuwa na miaka 73, ametamani yasiyomithilika.

Kwamba anatamani Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Burito Nyerere, aamke huko alikolala ili kuja kuadabisha watu wanaokichezea chama chake.

Raia huyo mstaafu wa jeshi, akiitwa Mzee Tai, mwenye makazi yake Kunduchi, Kinondoni, Dar es Salaam, amechefukwa na kauli na msimamo wa baadhi ya viongozi wa chama chake, Chama Cha Mapinduzi (CCM) alioidai wana-taka kuvunja katiba na kuleta tafrani – “kwa kuharibu chama.”

Mzee huyo amewaambia waandishi wa habari jana, kuwa endapo kuzimu kungekuwa kunafikika na kurejea juu ya uso wa dunia, basi angeenda “kum-omba Nyerere arejee atie adabu kidogo wakuda.”

Kwamba amekasirishwa mno na kauli ya Naibu Katibu Mkuu wa CCM-Zanzibar, Dkt. Mohamed Said Dimwa, ambaye eti anatamani Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi aongoze visiwa hivyo kwa miaka saba bila kufanyika uchaguzi.

Eti Dkt. Dimwa anasema kuwa kufanya uchaguzi mkuu mwaka kesho, 2025, ni kupoteza muda na rasilimali fedha, kwani Rais Mwinyi anatosha na kwamba miaka mitano ni kipindi kifupi sana kwa “watendaji wazuri.”

Mzee Tai akaeleza kuwa Dimwa amemkasirisha sana na amewaudhi wakongwe wengine wa siasa ndani ya chama chake, ambacho anadai kimejengwa kwenye misingi imara ya kufuata katiba na taratibu.

Mstaafu huyo akasema kuwa kush-

indwa kwake kumfuata Nyerere, kunamlazimisha sasa apande chombo (boti/meli) amfuate Dimwa ili akamtie adabu na kumuonyesha kwamba chama chao hakiende hivyo.

“Hivi huyu mtu anajiita daktari Dimwa katoka wapi, mbona simfahamu mie, au ni hawa vijana wa dotkomu, wanaotaka kuharibu chama changu?” Alihoji mzee huyu huku akitokomea kwa kusonya...”mmvyyyyiii.”

Tabasamu la “mabosi ledi...”



Mwakilishi Mkazi wa Taasisi ya Women Creating Wealth (WCW), Brenda Mihanjo (kushoto), akiwa na kiongozi wa taasisi hiyo nchini Tanzania, Anabahati Mlay, wakifurahia jambo kama walivyonaswa na kamera ya Pambazuko wiki iliyopita jijini Dar es Salaam. WCW inaendeshwa chini ya Wakfu ya Graca Machel.



Habari



Wafanyabiashara ya ng'ombe katika Mnada wa Pugu na mifugo yao wakisubiri wateja juzi. (Picha na Pambazuko).

Mnada Pugu wageuzwa shamba la bibi

● Kuna ufisadi wa kutisha, Vigogo wizarani wamo

Na Waandishi WETU

ZAIDI ya shilingi milioni 100 huingia – kila mwezi, mifukoni mwa watumishi wasiokuwa waaminifu wa Mnada wa Kimataifa wa Mifugo uliopo Pugu, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam – kwa njia ya wizi wa fedha za umma.

Wizi huo hufanywa kupitia mtandao mkubwa wa rushwa ukishirikisha watumishi wa mnada na baadhi ya vigogo waandamizi kutoka wizara husika, Pambazuko linaeleza kinaga ubaga.

Uchunguzi wa Pambazuko uliofanyika kwa kupiga kambi maeneo yanayohusika – kwa siku 13, umebaini kuwa mnada huo, ambao upo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, umegeuka kuwa chumio na kichaka cha watumishi wasiokuwa waaminifu ambao wamekuwa wakijipatia mapato yasiyokuwa halali.

Uchunguzi huo umegundua kuwapo kwa mianya ya 'upigaji' unaotekelezwa kupitia vibali vya kusafirisha mifugo unaofanywa na watumishi wa mnada huo kwa upande mmoja pamoja na wafanyabiashara wa mifugo kwa upande mwingine.

Chini ya utaratibu huo wa kifisadi, kikundi hicho kimekuwa kikichepusha baadhi ya magari ya mifugo kabla ya kulipiwa ushuru wa serikali na wao kujichukulia fedha hizo.

Kwa kawaida - na kisheria, kila ng'ombe anayeletwa mnadani hapo hutozwa shilingi 7,500 ikiwa ni ushuru.

Kati ya hizo; shilingi 1,000 hutozwa kwa kila ng'ombe kwa ajili ya ushuru wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na shilingi 6,500 zinazosalia huingizwa kwenye mfuko wa serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Kwa upande wa mbuzi, ushuru wake ni shilingi 3,000 ambapo halmashauri hiyo ya jiji huchukua shilingi 500 kwa mbuzi mmoja na shilingi 2,500 ni mapato ya serikali kupitia wizara husika.

Chanzo cha habari mnadani hapo kimeambia Pambazuko kuwa, kwa siku mnada huo unapokea ng'ombe kati ya 800 hadi 1,300 na baada ya ng'ombe kuuzwa, hupelekwa katika machinjio mbalimbali jijini Dar es Salaam.

Pia, mnada huo unapokea kati ya mbuzi 600 na 1,200 kutegemea msimu wa sikukuu za dini

Mnada Pugu wageuzwa shamba la bibi

Inatoka Uk. 6

ambapo kitoweo hicho uhitajika zaidi.

Chanzo hicho kimeeleza kuwa baadhi ya magari yanayoingia mnadani hapo, yanatofautiana ukubwa - ambapo baadhi hubeba wastani wa ng'ombe 40, 50 hadi 80 na kwamba magari mawili hadi matatu, kwa siku huchepushwa na makusanyo yote huingia mifukoni mwa mafisadi hao mnadani hapo.

Aidha, inadaiwa kuwa kati ya ng'ombe 100 mpaka 150, wanaingia mnadani bila kuwa na vibali ingawa wakati mwingine kibali kimoja hutumika kusafirisha mifugo zaidi ya mara moja kinyume cha utaratibu.

"Vibali vinavyotumika kusafirishia mifugo vinatolewa huko inakotoka mifugo kuja mnadani Pugu, lakini kibali kimoja kinaweza kutumika hata kwa safari tatu...

"Yaani, baadhi ya watumishi wamekuwa wakipitisha magari yaliyobeba mifugo kinyemela bila malipo halali na kumalizana na wasafirishaji pembeni," kimesema chanzo chetu na kuongeza:

"Kuna ng'ombe wanaoingia 900, 1200 hadi 1300 kila siku usiku, ina maana magari yanaanza kuingia saa nne usiku, na idadi ya soko la mbuzi inategemeana msimu, japokuwa kwa kawaida

wanaingia mbuzi 600 hadi 800 - lakini sikukuu zikikaribia, wanaingia hadi 2,000.

"Utaratibu ni kwamba ng'ombe wakishaingia mnadani usiku, wanapokelewa na askari na madaktari wa zamu wanaokesha, wanakagua vibali na afya za mifugo na kukuelekeza sehemu ya kuwahifadhi ili wapumzike maana watauzwa kesho yake asubuhi na mchana...

"Eneo hilo la ukaguzi, ndipo mahali penye rushwa, kwani kwa siku magari 20 hadi 25 hukaguliwa yakiwamo yale ambayo hayana vibali. Hapo kila gari wanakusanya shilingi 30,000 na wakati mwingine dau linapanda hadi shilingi 50,000.

Imebainika kuwa katika mgawo wa fedha zinazopatikana kila siku, wamo baadhi ya maofisa waandamizi kutoka wizarani wanaonufaika kwa ufisadi huo unaokosesha mapato kwa serikali.

Gharama ya wizi huo

Kiasi cha shilingi milioni 100 kinachoibwa kila mwezi, kikizidishwa kwa mwaka mmoja, jumla ya shilingi bilioni 1.2 huingia mifukoni mwa wezi hao.

Inaendelea Uk. 8



Waziri wa Mifugo na Uvuvi,

Taa zenye mwanga hafifu zikiwa zimefungwa baada ya agizo la Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega



Habari

Mnada Pugu wageuzwa shamba la bibi



Mkuu wa Mnada wa Ng'ombe wa Kimataifa Pugu, Noel Byamungu, akizungumza katika mahojiano maalum na waandishi wa habari wa gazeti la Pambazuko, Dar es Salaam (Picha na Fidelis Felix)

Inatoka Uk. 7

Endapo kiasi hicho kingeingia Hazina, kingekuwa na uwezo wa kuchangia mabweni 25 ya wanafunzi, au hata mahanga 17 ya wanajeshi wanapokuwa kwenye kambi kwa ajili ya mafunzo, lakini sasa fedha hizo zinaishia kwa wachache.

Kiasi hicho pia cha shilingi bilioni 1.2, kingeweza kujenga barabara ya kilomita moja kwa kiwango cha lami.

Aidha, fedha hizo zinazoishia mifukoni mwa watu wachache, zingeweza kukamilisha ada ya wanafunzi 37 wa udaktari - kwa miaka mitano katika Chuo Kikuu cha Kumbukumbu Hubert Kairuki, Dar es Salaam.

Mwanafunzi wa udaktari chuoni hapo hulipa shilingi milioni 33 kwa miaka yote mitano ya mafunzo yake.

Watumishi na Upatu

Gazeti la Pambazuko ambalo lilipiga kambi ndani ya mnada huo, limeshuhudia mchezo wa upatu unaochezwa na wezi hao wa fedha za

umma.

Imebainika kuwa watumishi wa mnada huo wana mchezo wa kupeana fedha kwa kila siku ambapo wanachangiana kati ya shilingi 100,000 hadi, 200,000.

Kipato hicho ni kikubwa mno kwa watumishi wengi wa serikali kukimudu, kwani ujira wa watumishi wa serikali wanaofikia kiapo cha shilingi 200,000 – kwa siku, ni kuanzia ngazi za mawaziri.

Uchuguzi wa Pambazuko umetambua kuwa mtumishi wa ngazi za wakaguzi katika mnada huo, anapokea mshahara usiozidi shilingi 785,000 kwa mwezi.

Hivyo, kuchangishana hadi shilingi 200,000 kwa siku, ni kuhalalisha wizi unaofanywa na watumishi hao.

Waziri Ulega apuuzwa

Tuhuma kuhusiana na kikundi hicho cha upigaji zilimfikia Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ambaye Januari 3, mwaka huu, alimuagiza Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Daniel Mushi, kuuondoa uongozi mzima wa Mnada wa Pugu kwa kile alichosema wameshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato katika mnada huo.

Waziri Ulega alitoa maagizo hayo jijini Dar es Salaam, alipofanya ziara katika mnada huo siku hiyo, kwa lengo la kukagua na kubaini changamoto zinazowakabili wafanyabiashara katika mnada huo.

“Naibu katibu mkuu, ondoa uongozi mzima wa hapa mnadani, kuanzia msimamizi mkuu na wengine wote, leta watu wengine na hao wengine utakaowaleta, uwape miezi sita kisha uniletee tarifa kama wanakidhi viwango.

“Nilileta timu hapa Desemba ikafanya kazi ya kukusanya mapato katika mnada huu, ndani ya siku 11, walikusanya zaidi ya shilingi milioni 100 na hii inaonyesha wazi katika mnada huu mapato ni makubwa ila kuna baadhi ya watu wanajinufaisha,” alisema Waziri Ulega.

Mbali na mnada huo kushindwa kufikia lengo la serikali la kukusanya shilingi milioni 200, Waziri Ulega pia aliagiza watumishi 15 wa mnada huo,

Mezani kwa Chahali

ALHAMISI iliyopita, Waingereza walipiga kura katika uchaguzi mkuu ulioishia kwa chama tawala Conservatives kubwaga vibaya na kulichokuwa chama kikuu cha upinzani cha Labour.

Kufuatia matokeo hayo, aliyekuwa waziri mkuu na kiongozi wa Conservatives, Rishi Sunak, alijiuzulu, na kiongozi mkuu wa Labour, Sir Keir Starmer kurithi nafasi hiyo.

Anguko la Conservatives halikuwa tukio la siku moja, kwa maana kwamba halikutokea tu siku ya uchaguzi. Anguko hilo lilojitengeneza kwa miaka kadhaa na ilikuwa ni suala la lini, na wala siyo endapo, chama hicho kingeng'oka madarakani.

Sababu za anguko la chama hicho ni nyingi, lakini baadhi ni hizi ni pamoja na kuchokwa kwa chama hicho, kwamba kwa miaka 14 ya utawala, wapiga kura walichoka na utawala wake.

Kuendelea kuibuka kwa skandali kadhaa ikiwamo ile ya "Partygate" ambapo mmoja wa viongozi wake waandamizi, Boris Johnson alikutwa na hatia za kusigina miongozo iliyozoeleka, zilisababisha kupotea kwa imani ya umma.

Hali mbaya ya uchumi nayo ni sababu nyingine iliyobebwa na wengi kwamba ilichochea na "uzee" wa chama hicho kuongoza.

Kuibuka kwa chama kingine cha Reform UK, kunaelezwa kuvutia wanachama na wapigakura wengi kutoka kwa Conservative.

Kitu kingine ni kuwepo kwa mabadiliko makubwa ya kiutendaji na mfumo ndani ya Chama cha Labour ambayo yalionekana na kuaminiwa kuwa yataleta mabadiliko kwa kuisimamia serikali mpya.

Funzo kwa CCM

Kama ambavyo Waingereza waliichoka Conservative, na hatimaye wakafanikiwa kuing'oa ndani ya sanduku la kura, siyo siri kuwa nchini Tanzania, wananchi wengi wameichoka CCM, na wakipata fursa ya kuitokomezwa mbali, hawatoshindwa kufanya hivyo.

Na kama Conservatives walivyojawa na kiburi kiasi kwamba hawakuona umuhimu wa kusikiliza vilio vya wananchi, ndivyo ambavyo CCM imekataa katakata kusikiliza vilio vya Watanzania wengi na imegoma kubadilika.

CCM inaamini kuwa mizizi yake na mbinu

Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com



Chadema, ACT mmesoma ukuta wa Labour?

zahila upata ushindi mar azote, itachukua miaka mingi kuondolewa madarakani kupitia sanduku la kura.

Mazingira yanayokipendelea chama hicho na ambayo yamekiwezesha kushinda chaguzi zote tangu mfumo wa vyama vingi uanzishwe mwaka 1992, bado yapo na yayumkinika, kuamini kuwa yataendelea kuwepo kwa muda mrefu.

Dhahiri ni kwamba ushindi wa Labour ulichangiwa na upungufu wa kiutendaji wa Conservatives badala ya uimara wa chama hicho kilichoshinda jana, na hivi ndivyo inavyokwenda kutokea hata Tanzania.


Funzo kwa Chadema na ACT-Wazalendo ni kwamba vyama hivi vina mtaji mkubwa kama waliokuwa nao Labour ya Uingereza.

Labour ilifanikiwa kujenga maelezo ya kuaminika kwa umma kwamba matatizo ya nchi yao yanatokana na upungufu wa Conservatives, na hili liko ukutani kwa vyama vya upinzani Tanzania.

https://instagram.com/evarist_chahali



Waziri Mkuu wa Uingereza, Sir Keir Starmer



Tafakuri ya Bagonza

Ujinga ni mzigo vs ujinga ni mtaji



Na Dkt. Benson BAGONZA

JULAI 6, 2024, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe, Kagera, imehitimisha kundi la pili la watu wazima 125 katika kisomo cha watu wazima (EWW).

Kundi la kwanza lilihitimishwa mwaka jana, 2023. Watu wazima wasiojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK), sasa wanapata fursa ya kuelimishwa kupitia mradi maalum katika Jimbo la Murongo, Tarafa ya Murongo-Kyerwa.

Katika kuonyesha uthibitisho wa kukamilisha masomo hayo, wahitimu wamepewa vyeti vya kuhitimu.

Mradi huu unafadhiliwa kwa ushirikiano na Shirika la Bread for the World la Ujerumani, huku majimbo ya Murongo (Tanzania) na Gutersloh (Ujerumani), wakiwa ndio watekelezaji wa mradi huu.

Labda kama kuna takwimu za kipekee, lakini kwa macho yangu naona ujinga unaongezeka katika maeneo mengi ya vijijini.

Tulizoea kusema ujinga ni mzigo lakini sasa ujinga ni mtaji kwa makundi kwa makundi

mbalimbali, kama ambavyo yanaainishwa hapa.

Kwamba lipo kundi la viongozi wa dini; hawa wanahitaji wajinga wengi ili wawauzie wokovu, utajiri hewa, uponyaji na mambo mengine kupitia imani.

Kwamba wanasiasa nao wanahitaji wajinga wengi ili wawadanganye bila kukamatwa na wawajaze ahadi hewa.

Kwamba lipo kundi la waganga wa kienyeji, hawa wanahitaji wajinga wengi wa kuwaletea kuku, mbuzi na ng'ombe, huku hao wajinga wakilishwa vinyesi na mikojo.

Kwamba kuna kundi jingine la walimu, hawa wanahitaji wajinga wengi ili wafanye mazoezi ya kufuta ujinga kwa kuuongeza.

Kwamba lipo kundi la watumishi wa serikali wasio waaminifu, hawa wanahitaji wajinga wengi ili wawatoze rushwa na kuwauzia haki zao.

Kwamba lipo kundi la wahisani na Wafadhili, ambalo linahitaji wajinga wengi ili wapate pa kupeleka misaada inayodumaza na kuwasaidia kumiliki uchumi wa wajinga.

Kwamba kundi jingine ni Serikali, ambapo hili linahitaji wajinga wengi ili waiogope. Kwa kawaida serikali huwaogopa wananchi wanaojielewa.

Kwamba kundi jingine ni matapeli wa mitandaoni, ambalo linahitaji sana wajinga wengi ili liweze kutajirika bila kufanya kazi.

Kwamba kuna kundi la wafanya biashara, ambalo linahitaji wajinga wengi wanaoamini kwamba kuna duka la bei nafuu.

Kwamba kuna kundi jingine la umaskini na maradhi, ambalo linahitaji kuwa na wajinga wengi ili hawa ndugu waendelea kustawi.

Sasa ielweke kuwa vita ya kupambana na ujinga haijaanza. Ikianza mniamshe. Hakuna kundi lisilo na mjinga.

Ukichunguza kundi usimuone mjinga, tambua wewe ndiye mjinga.

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kilutheri la Kiinjili Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa makala ndani ya Pambazuko.



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Ni aibu kubwa Dar es Salaam kukosa maji



UKOSEFU wa maji katika jiji kubwa la Dar es Salaam ni suala linalotia hofu na kuchanganya, hasa ikizingatiwa kuwa jiji hilo ni kitovu cha biashara.

Taarifa iliyotolewa wiki iliyopita wakati wa ziara ya Waziri wa Maji, Jumaa Aweso inafichua changamoto nyingi zinazoikumba Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (Dawasa), hususan katika kuwajibika na utendaji wa viongozi wake.

Katika ziara hiyo aliyoifanya Aweso, alichukua hatua kali kwa kusimamisha kazi viongozi wakuu wawili wa Dawasa, ambao ni Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu, Kiula Kingu na Mkurugenzi wa Uzalishaji na Usambazaji Maji, Shaban Mkwanywe.

Hatua hii ilichukuliwa baada ya kugundua kuwa maagizo yake yamepuuzwa na kwamba kuna uzembe katika matengenezo ya miundombinu muhimu ya maji.

Uzito wa hali hii unaonekana katika malalamiko ya Aweso kuhusu kutokuwepo kwa viongozi hao kwenye ziara muhimu za waziri, jambo ambalo linaashiria ukosefu wa nidhamu na uzalendo miongoni mwa watendaji wa Dawasa.

Swali kuu linalojitokeza ni kuhusu uzalendo na ufanisi wa watendaji wetu. Inaonekana kuna pengo kubwa katika kujali maslahi ya umma na kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu.

Jiji la Dar es Salaam, likiwa na vyanzo vya maji vya kutosha na miundombinu inayohitajika, linapaswa kuwa mfano wa utoaji wa huduma bora za maji.

Hata hivyo, tatizo la ukosefu wa maji linaendelea, hali inayoweza kutafsiriwa kuwa ni hujuma dhidi ya serikali na wananchi wake.

Hatua ya Aweso ni ya kupongezwa kwani inaashiria umuhimu wa uwajibikaji katika utumishi wa umma.

Hata hivyo, inafaa kuzingatia kuwa kusimamisha kazi viongozi ni hatua ya kwanza tu, hivyo ni muhimu kufuatilia kwa karibu uchunguzi unaotarajiwa kufanyika ili kubaini chanzo halisi cha tatizo na kuhakikisha kuwa wale wote waliohusika wanawajibikwa ipasavyo.

Sambamba na hatu hiyo, serikali inapaswa kuimarisha mifumo ya usimamizi na uwajibikaji ili kuhakikisha kuwa hali kama hii haitokei

tena.

Ifahamike kuwa changamoto za maji jiji ni Dar es Salaam zinatoa picha mbaya kuhusu ufanisi wa watendaji wa Dawasa na kwamba ni aibu kubwa kuona jiji hilo likikosa maji huku vyanzo vya maji, miundombinu, na rasilimali nyinginezo zikiwa zipo.

Ni wakati sasa wa serikali kuchukua hatua madhubuti zaidi kuhakikisha huduma za msingi zinatolewa kwa ufanisi na kwa wakati kwa wananchi wake.

Serikali inapaswa pia kuangalia uwezekano wa kuwajenga watendaji wake ili wawe na uzalendo na kujitolea kwa dhati katika kutumikia nchi yao.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com



Uchambuzi



Mbunge wa Kisesa, Luhaga Mpina

Mpina ameanza safari au anafika mwisho?

Na Mwandishi WETU

LUHAGA Mpina, mbunge wa Kisesa ameamua kuwa tofauti.

Ameamua kwenda mahakamani, akipinga adhabu ya Spika, pia kumshitaki Waziri wa Kilimo Hussein Bashe ambaye tuhuma dhidi yake zimemsababishia adhabu ya kutohudhuria vikao 15 vya bunge.

Historia inaonyesha kuwa tangu alipoingia bungeni mwaka 2005, Mpina haikuwahi 'kubweteka' wala kutulia kama ilivyo kwa wabunge wengine wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambao wamekuwa wakipitisha kiulaini na kuunga mkono karibu kila hoja inayoletwa mbele yao na serikali.

Ikumbukwe kwamba bunge la baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2005, yaani Bunge la 11, lilikuwa na kambi thabiti ya upinzani kukiwa na wabunge 111 kati ya wabunge 374.

Katika idadi hiyo, CCM ilikuwa na wabunge 263 akiwemo Mpina, ambaye angeweza kuende-

lea kupata stahiki zake kama mbunge wa CCM kwa kuunga mkono hoja tu, bila kupata bughudha yoyote.

Lakini haikuwa hivyo, Mpina alijenga misimamo yake ya kuinyoosha serikali akiwa mbunge wa chama tawala.

Kutokana na misimamo yake, alipata upinzani kutoka kwa wabunge wenzake, lakini hakurudi nyuma. Aliendelea na haiba hiyo katika mabunge yote.

Mmoja wa marafiki wa karibu wa Mpina anasema kwa hatua yake ya kuamua kwenda mahakamani kama alivyoazimia na kutangaza rasmi Juni 29, mwaka huu, baada ya kupewa adhabu na Bunge - kwa siasa za CCM atatengwa, na anaweza fukuzwa uanachama.

Muhimu awe na "plan B" ili iwapo atafukuzwa CCM, ajue atakwenda wapi, kwa kuwa hatakosa ubunge iwapo ataamua kusimama kidete.

"Ila sidhani kama ataweza kufanya siasa nje ya CCM, ni wanaCCM wachache sana wanaweza kufanya siasa nje ya CCM....

"Kumbuka siasa zetu siyo wananchi wenye maamuzi, bali dola ndio yenye maamuzi. Mfano rahisi hadi sasa wameshamzuia kuingia bungeni, na kama akienda mahakamani, sijui kama itamsaidia sana, ila ajipange sawasawa," alisema.

Rafiki huyo wa karibu wa Mpina alisema hata

Kona ya Dkt. Bisimba

Na Dkt. Hellen Kijo
BISIMBAHifadhi zizingatie
haki za binadamu

NILIBAHATIKA kuhudhuria uzinduzi wa taarifa ya kiuchunguzi kuhusu haki za binadamu na uhifadhi.

Uzinduzi huo uliletwa kwetu na Shirika la Centre for Strategic Litigation wakiwa pamoja na Media Brains na SK Media.

Walifanya uchunguzi nchi nzima ya Tanzania na taarifa hiyo ilikuwa ikieleza matokeo ya kazi hiyo.

Taarifa hii ilikumbushia hali ya uvunjifu wa haki za binadamu uliowahi kutokea miaka ya nyuma wakati wa operesheni za kulinda hifadhi za wanyama zilizojulikana kama "Operesheni Uhai" na "Operesheni Tokomeza".

Uhai ilikuwa na lengo la kuzuia uwindaji wa tembo na biashara ya meno ya tembo wakati Tokomeza ilinulia kutokomeza ujangili uliokuwa unatendeka ndani ya Hifadhi za Taifa.

Operesheni hizi zililaumiwa sana kwa ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu hadi mawaziri waliokuwa na dhamana wakajiuzulu.

Lililoshangaza ni kuwa pamoja na yaliyojitokeza katika operesheni hizo, bado kama taifa hatujaweza kujifunza na kufanya uhifadhi kwa kuzingatia haki za binadamu.

Swali kuu ambalo linapaswa kuulizwa katika uhifadhi ni wapo uhifadhi upo kwa ajili ya nani? Je, ni kwa ajili ya wanyama au ni kwa ajili wa watu?

Inasemekana theluthi moja ya ardhi ya Tanzania imetengwa kuwa Hifadhi za Taifa. Hili ni jambo jema, ila inabidi ifahamike kuwa ardhi huwa haiongezeki ila watu ndiyo huongezeka.

Kwa takwimu za mwaka 2022, ongezeko la watu Tanzania ni asilimia 3.0 kwa mwaka.

Tulipopata uhuru mwaka 1961 na watu waliokuwepo Tanganyika, wakati huo ni milioni tisa. Hivi sasa watu waliopo wanakaribia milioni sitini.

Ardhi iko vilevile na ndiyo maana katika uhifadhi, ni lazima suala la haki za watu lizingatiwe sana.

Taarifa iliyozinduliwa inaonyesha jinsi ambavyo watu huondolewa sehemu zao za asili ili kupisha uhifadhi.


Katika kuondolewa, ushirikishwaji ni mdogo au haupo kabisa. Wapo watu ambao huondolewa bila kulipwa fidia, wapo wanaopewa fidia isiyokidhi na wapo wanaoondolewa bila kupewa eneo mbadala. Wapo wanaopigwa na kuumizwa pia.

Kuna ushahidi uliotolewa wakati wa utoaji wa taarifa hii wa jinsi ambavyo wananchi wamekuwa ni wahifadhi wa asili na hizi hifadhi zilizokuja kutambuliwa baadaye.

Wapo wananchi wanaoishi kuzunguka hifadhi, ambao maisha yao yanategemea rasilimali katika hifadhi hizo, lakini wamejikuta hawawezi kabisa kutumia rasilimali hizo.

Pamoja na kuwa na umuhimu wa kuihifadhi ardhi na mali asili zilizo mo ikiwepo misitu, wanyama na mazingira kwa ujumla, uhifadhi wenye tija ni ule unaozingatia ubinadamu na kuwashirikisha watu ambao uhifadhi huo ni kwa ajili yao na siyo vinginevyo.

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.



Habari

Mnada Pugu wageuzwa...

Inatoka Uk. 8

wahamishwe kwa kuwa wana mtandao wa watu wanaofuja mapato ya serikali.

Hata hivyo, Pambazuko linazo taarifa kuwa watumishi waliohamishwa kwenye mnada huo upande wa mbuzi ni wanne na kwa upande wa mnada wa ng'ombe ni wanane.

Hata hivyo, wengine ambao ni vinara wa upigaji mnadani hapo, hawajaguswa na hatua hiyo. Kati ya idara ambazo hazijaguswa ni pamoja na idara ya uhasibu ambako kunaelezwa kuwa ndiko kwenye mzizi wa upigaji huo.

Kabla ya ziara ya Waziri Ulega, wizara hiyo ilikuwa imeweka malengo ya kukusanya shilingi milioni 200 kila mwezi kutoka kwenye mnada huo.

Serikali ilipeleka timu iliyofanya kazi kwenye mnada huo kwa siku 11 na iliweza kukusanya zaidi ya shilingi milioni 100 ndani ya siku 11, jambo ambalo linadhihirisha wazi kuwa kuna wizi mkubwa wa mapato.

“Kwa muda wa siku 11 tu, kiwango hicho cha fedha kilikusanywa na timu hiyo. Kwa hiyo, ni wazi kwamba mnada huo unao uwezo wa kukusanya zaidi ya shilingi milioni 300 kila mwezi” kilisema chanzo hicho.

Wakati wa ziara hiyo Waziri Ulega pia alim-uagiza naibu katibu mkuu, kuhakikisha anakagua minada yote mikubwa nchini na kuangalia

utendaji wa minada hiyo na kumtaka achukue hatua pale panapostahili ili kuboresha shughuli za sekta ya mifugo nchini.

Aidha, waziri huyo alitumia nafasi hiyo kumuelekeza naibu katibu mkuu huyo, kuhakikisha ndani ya wiki moja ukuta uliodondoka katika mnada huo unajengwa pamoja na kufanya ukarabati wa miundombinu ili kuboresha mazingira ya mnada.

Katika ziara hiyo ya waziri, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Pugu Stesheni, Shukuru Mwinjuma, alitaja changamoto ya wafanyabiashara wadogo kukamatwa na mifugo yao kwa madai kuwa siyo halali wakati wana vibali vina-vyotakiwa.

Mwinjuma alitaja changamoto nyingine kuwa ni uhaba wa maji unaosababishwa na mgawo wa maji na ubovu wa barabara ya kuingia mnadani hapo.

Mkuu wa mnada

Pambazuko lilimtafuta Mkuu wa Mnada wa Pugu, Noel Byamungu, ambaye aliwaeleza waandishi wetu kuwa maagizo ya Waziri Ulega yame-shatekelezwa kwa kiasi kikubwa na mnada huo unafanya kazi kwa saa 24.

“Tumefunga taa tano ambazo ndizo zinazotumika muda wote unapohitajika na vituo vyetu humu ni vitano na kila kituo kina taa kubwa. Lakini, mara nyingi tunamulika wanyama waliopo na sehemu za kushushia na kupakizia wanyama,” alisema.

Hata hivyo, uchunguzi uliofanywa na Pambazuko umebaini kuwa taa hizo zinazosemwa na Byamungu zilikuwapo hata kabla ya ziara ya Waziri Ulega.

Aidha, kikosi cha Pambazuko kilishuhudia ng'ombe wakipakizwa kwenye malori gizani bila udhibiti wowote kutoka kwa uongozi wa mnada huo.

Kuhusu suala la maji ya uhakika katika eneo hilo, Byamungu alisema miundombinu ya maji iko tayari ingawa sasa hayapatikani kwa uhakika kwa kuwa wanategemea maji kutoka Dawasa ambayo yanapatikana kwa kiasi kidogo.

“Kwa sasa tunasubiri mradi mkubwa wa maji wa Dawasa ambao tayari umeshazinduliwa na



Lambo la kunyweshea mifugo lililopo ndani ya mnada wa Pugu lilikiwa halina maji. (Picha na Fidelis Felix)



Mnada Pugu wageuzwa...



Muonekano wa taa zenye mwanga hafifu zilizofungwa ndani ya mnada wa Pugu. (Picha na Fidelis Felix)

Inatoka Uk. 14

mkuu wetu wa Mkoa wa Dar es Salaam, utakapokamilika tutapata uhakika wa maji ya kutosha kwenye mnada huu...

“Tatizo katika eneo hili hakuna uhakika wa maji, hivyo tumechimba visima karibu vitatu, lakini eneo hili halina maji...”

“Kuna kisima kirefu cha karibu mita 300 ambacho kilichimbwa katikati ya eneo la mnada, lakini hakina maji kabisa kutokana na asili ya eneo hili halina maji...”

“Agizo ambalo halijatekelezwa kabisa ni la ujenzi wa barabara ya kuingia mnadani hapa ambayo inatakiwa kujengwa na Wakala wa Barabara (Tanroads),” alisema.

Makusanyo

Kuhusu makusanyo, alisema kwa sasa wana makusanyo ya karibu shilingi milioni 250 kwa mwezi, lakini taarifa zaidi ziko kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Kwa mujibu wa Byamungu, kwa siku, wanaingiza wastani wa ng’ombe 800, japokuwa wakati mwingine inategemeana na msimu.

Kwa upande wa mbuzi katika kipindi cha msimu wa kuchinja, alisema wanafikia hadi

mbuzi 1,000, lakini katika vipindi vya kawaida, wanapokea mbuzi kati ya 200 hadi 300.

Alisema yeye husimamia utozaji wa shilingi 6,500 kwa kila ng’ombe ambazo hupelekwa wizara na kwa mbuzi, hukusanya shilingi 2,500 kwa ajili ya wizara.

Kuhusu mapato ya jiji, alisema husimamiwa na maofisa wengine ambao hawezi kuwasemea.

Hata hivyo, Pambazuko limebaini kuwapo kwa mvutano na misugvano ya kimaslahi kati wakusanya ushuru wa wizara pamoja na wale wa Jiji la Dar es Salaam ambapo wanatuhumi ana kwa mambo mbalimbali.

Chanzo cha msugvano huo kimetajwa kuwa ni ukusanyaji wa mapato kwa upande zote mbili kutokana na wafanyakazi wa jiji kusimamia ipasavyo mapato yao na kusababisha kuwapo kwa tofauti kubwa ya idadi ya wanyama wanaolipiwa ushuru mnadani hapo ikilinganishwa na wale wanaokusanya hesabu za wizara.

Uchepushaji wa ng’ombe

Kuhusu uchepushaji wa ng’ombe kama ilivyo-oshuhudiwa na Pambazuko, Byamungu alisema siyo jambo rahisi kwa kuwa mfumo unaosoma vibali ndiyo unaosoma stakabadhi zinazolipwa kwa jiji na zile zinazolipwa kwa wizara.

“Kimfumo, wizara ikitoa vibali kwa ng’ombe 50 hakitakamilika bila kusoma kuwa jiji nalo limetoa ng’ombe 50. Kwa kifupi ni kwamba, ili upokelewe machinjioni, lazima uwe na vibali hivyo na hutaweza kuchinja kama huna vibali...”

“Hii maana yake ni kwamba, chochote kita-kachokuwa kimepungua, kule itabidi uchajiwe upya au upigwe faini. Sasa hivi wafanyabiashara wengi hawapendi faini, kwa hiyo, mara nyingi utakuta utii wa sheria bila shuruti ni kama ume-ongezeka...”

“Kuhusu mapato, ukioanisha lengo lililopita, utaona kwamba sasa hivi kuna ongezeko la karibu mara mbili na nusu. Kwa hiyo, kama zamani walikuwa wanachepusha, sasa wamedhibitiwa ndiyo maana tuna matokeo kama hayo,” alisema.

Hata hivyo, maelezo hayo ya mkuu wa mnada yanakinzana na maelezo ya vyanzo vyetu vinavyoeleza kuwa, utoroshaji wa mifugo in-

Habari

Sumaye: Magufuli nusura azamishe...

Inatoka Uk. 4

pia anawaonya, ni tofauti na huko tulikotoka...”

“Kwa hiyo mimi nasema anaenda vizuri, watu wana amani, watu wanafanya kazi zao kwa utulivu, kuna mambo ya hapa na pale ambayo unaweza kusema labda hilo liko hivi ama vile, lakini kwenye utawala hayakosekani,” amesema Sumaye.

Kwenye uchumi

Akizungumzia uchumi, Sumaye anasema walipomaliza kipindi chao cha utawala chini ya Rais Mkapa, waliondoka wakiiacha nchi ikiwa madhubuti kwenye uchumi mkubwa (macro economy).

“Wakati tunaingia hali ilikuwa ngumu sana,” amesema na kubainisha kuwa katika utawala wao pamoja na kuweka msisitizo kwenye ujenzi wa uchumi mkubwa, lakini pia hawakuacha kushughulika na uchumi mdogo (micro economy)...”

“Miaka mitano ya mwanzo hali ilikuwa mbaya sana, wakati tunashughulika na macro economy na kama mtakumbuka wananchi walikuwa wameanza kusema kwamba Mkapa amelea ukapa, lakini actually (kwa hakika) tulikuwa tunarekebisha uchumi na kurekebisha uchumi unaanza na macro economy (uchumi mkubwa) ili zile nguzo kuu za uchumi ziwe imara...”

“Sasa ukishaweka zile nguzo imara baadaye kuja kuweka nyama inakuwa rahisi na micro tulikuwa hatujaiacha, na kama mtakumbuka ndio maana walikuwa wanasema wakati wa Mkapa hata bei za vitu zilikuwa zimetulia sana, zilikuwa hazirukiruki, ni kwa sababu tulikuwa tumejielekeza kwenye upande wa macro,” alisema.

Amesema pamoja na kwamba waliacha nchi katika uchumi mzuri, lakini haelewi kilichokuja kuvurugika kiasi cha uchumi mdogo kuendelea kuwa na matatizo hadi leo.

“Labda wazungumzie viongozi waliofuatia na waseme nini kiliharibika,” ameongeza Sumaye ambaye aliingia kwenye uwaziri mkuu

akiwa na umri wa miaka 45 na kutoka akiwa amefikisha miaka 55.

Mifumo mibovu

Sumaye amesema kitu kikubwa kinachoitesa Tanzania na nchi nyingi za Afrika kwa sasa, ni kukosekana kwa mifumo imara ya kuendesha nchi.

Amebainisha kwa mfano kuwa nchi inapaswa kuongzwa na mpango wa maendeleo wa tafa, lakini hakuna mfumo wa kisheria wa kuulinda mpango huo ili kuhakikisha unatekelezwa kikamilifu.

Sumaye akasema hali hiyo inasababisha kila kiongozi anayeingia madarakani kufuta mipango iliyokuwa inafanywa na kiongozi aliyemtangulia, na kuanzisha mambo mapya.

“Unakuta kuna mipango mizuri na inaelekea pazuri, lakini anakuja kiongozi mwingine anaiweka pembeni, halafu anaanza mipango yake mingine mipya kwa hiyo hilo ni tatizo kwa nchi nyingi za Afrika...”

“Mimi nakumbuka mzee Mkapa aliwahi kusema kwamba tatizo mtu ukishatoka madarakani, hakuna anayetaka tena kukutumia wala kukuuliza jambo lolote na akasema kwamba nataka niwaambie wenzenu huko nje wanatufaidi sana na kututumia, lakini huku ndani sisi tunaonekana hatufai kwa hiyo kuna hilo tatizo katika Afrika, sijui tatalifanyeje na siyo awamu moja ni karibu kila awamu ina tatizo hilo,” amesema.

Sumaye akabainisha kuwa tatizo hilo linasababishwa na nchi nyingi za Afrika kutokuwa na taasisi zenye nguvu, bali watu wenye nguvu.

Inaendelea Uk. 17



John Magufuli

Sumaye: Magufuli nusura azamishe...



Inatoka Uk. 16

Alipoulizwa kuhusu jambo analojivunia wakati akiwa mtendaji mkuu wa serikali, akajibu kwa kujiamini; “chini ya Rais Mkapa tulifanikiwa kujenga taasisi nyingi na kuzifanya kuwa na nguvu kuliko watu.”

Ameeleza kusikitishwa kwake kwa taasisi hizo kuja kupoteza mwelekeo baada ya wao kuondoka madarakani na kwamba hadi sasa nyingi ya taasisi hizo zinazidiwa na nguvu za viongozi, hasa wanasiasa.

“Bila taasisi zenye nguvu hata kwenda kwenye uchumi wa ushindani huwezi kwenda, inakuwa ngumu,” akaongeza waziri mkuu huyo mstaafu.

Waziri mkuu huyo wa kwanza wa Bunge la vyama vingi, amesema pia katika uongozi wao walifanikiwa kusimamia ukuaji wa demokrasia, akisema bunge la wakati huo lilikuwa na nguvu.

Katiba mpya

Akijibu swali kwamba ili kurekebisha mifumo mizuri kama kuna haja ya kuwa na katiba mpya sasa, alisema hadhani kwamba Katiba mpya itaweza ikamzuia kiongozi mbaya kufanya mambo mabaya.

“Katiba mpya kwa lugha ni tamu, lakini Katiba mpya haiwezi ikazuia kiongozi mbaya kufanya mambo mabaya kama hii mifumo tunayoisema haina uwezo ya kumdhibiti...”

“Hata Katiba ya sasa kimsingi wametumia marais wote waliopita, ametumia Mwalimu Nyerere Julius- rais wa awamu ya kwanza), Ali Hassan Mwinyi (awamu ya pili), Mkapa (awamu ya tatu), Jakaya Kikwete (awamu ya nne).”

“Na pia awamu ya tano, ambapo wakati wa Rais Magufuli utawala ukawa kitu kingine tofauti na tawala zilizokuwepo, lakini katiba ni hiyohiyo kwa hiyo watu wasije wakafikiri kwamba katiba ndio mwarobaini wa kila kitu...”

“Kinachotakiwa ni mifumo iliyo na nguvu. Katika nchi za wenzetu mifumo inawekwa ambayo ina nguvu na rais hawezi kuamua kufanya kitu ambacho ni cha hovyoy kwa sababu mfumo utamzuia, sisi kwetu rais anaweza kuamua kufanya kitu cha hovyoy akitaka...”

“Bado nasema Katiba mpya inaweza kusaidia tu hapa na pale, lakini mifumo ni tofauti kidogo na Katiba, mifumo iko kwa utendaji zaidi, kwa mfano Marekani, rais wake hawezi kufanya kitu chochote kikubwa bila system (mfumo) kukubali na akitaka kufanya itamzuia na kumdhibiti na hana la kufanya,” akabainisha Sumaye.

Kashfa ya sukari

Akizungumzia kuhusu mgogoro wa sukari uliosababisha Mbunge wa Kisesa, Luhaga Mpinna, kusimamishwa kuhudhuria vikao 15 vya bunge, Sumaye amesema kuna tatizo kwa serikali kutowajibika katika hilo.

Sumaye ambaye alipata kuwa naibu waziri wa kilimo wakati wa uongozi wa Rais Mwinyi, akasema tangu wakati wa uongozi wao, utaratibu ulikuwa ni wenye viwanda wanaagiza sukari nje, wakati inapoadimika, lakini anashangazwa na kinachoendelea hivi sasa.

“Sitaki kuingia kwenye mzozo uliopo. Mimi nimekuwa kwenye kilimo siku nyingi, kwa maa-na nimekuwa naibu waziri wa kilimo, sukari siku nyingi imekuwa ngumu...”

“Utaratibu tuliokuwa nao zamani sasa sijui umebadilikia wapi, lakini utaratibu wa zamani ni kwamba wizara tunaangalia uzalishaji wa sukari nchini ni kiasi gani, ulaji ni kiasi gani, pengo ni kiasi gani...”

“Kwa hiyo wazalishaji wa ndani, wakifunga viwanda - kwa kawaida ni miezi mitatu, ndiyo tunahakikisha wakati huo sukari inaingizwa nchini...”

“Hata hivyo, baadaye utaratibu huu ika-

Inaendelea Uk. 21

Uchambuzi

Mpina ameanza safari au anafika mwisho?

Inatoka Uk. 12

kama wakifanikiwa kumfukuza CCM, hilo siyo tatizo kwa sasa baadhi ya watu wake wa kari-bu hawamshauri kugombea ubunge, bali wana-taka agombee urais kwa kuwa kwa alipofiki sasa ndiyo saizi yake na wananchi watakuwa na imani na usalama wa mali za nchi.

“Kwa sasa tayari ana wakati mgumu ndani ya CCM, tukumbuke taratibu za kugombea kuanzia udiwani hadi urais, kuna wajumbe wa kupitisha jina na wengi tunaomuunga mkono siyo wajum-be...”

“Hata hivyo, ikifikia hatua hiyo, muda ndio utakaoelekeza kuhusu hatua za kuchukua. Ngoja tuone watakachofanya hao wasiomtakia mema, ndo tujue nguvu ielekezwe wapi,” alisema rafiki huyo wa Mpina.

Safari yenye mashaka

Juni 24, mwaka huu Mpina aliadhibiwa kutohudhuria vikao 15 vya Bunge, kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kutokana na kutiwa hatiani na Kamati ya Maadili ya Bunge, kwa madai ya kudharau kiti cha Spika.

Kwa adhabu hiyo, Mpina hatohudhuria vikao vilivyobaki vya Bunge la Bajeti na hatahudhuria baadhi ya vikao vya awali katika bunge lijalo Novemba mwaka huu.

Mpina, mwanasiasa machachari anayeonekana kuwa mwiba kwa CCM na wabunge wenzake, aliibua sintofahamu kiasi cha bunge kutafuta namna ya kumshughulikia, baada ya kuwasilisha tuhuma kuhusu Bashe kutoa vibali vya kuingiza sukari nchini kinyume na utaratibu.

Mpina, mbunge tangu mwaka 2005 ni mwanasiasa mtulivu na anayejua kujenga hoja vyema, amekuwa miongoni mwa wanasiasa wanaojiamini, ambae kamwe harudi nyuma, aliyeaminiwa sana na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, John Magufuli.

Ni mwanasiasa anayejiamini na baada ya kuhudumu kama mbunge kwa miaka 10, mwaka 2015 alijitokeza kuchukua fomu ya kuomba uteuzi wa kuwa mgombea wa urais kupitia CCM.

Katika safari yake, Juni 2015 alikuwa mwanachama wa 11 wa chama hicho aliyechukua fomu



kati ya wanachama 43 waliojitokeza kuchukua fomu hiyo, akijinasibu kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani akiahidi kuja na njia mbadala za ukusanyaji mapato, japokuwa alikatwa katika hatua za awali.

Alijenga hoja kuwa iwapo Watanzania watampa dhamana, wizi, utoroshaji wa fedha za umma utafika mwisho, kama kuna watendaji wanaona hawawezi kuacha basi siku wakisikia anaapishwa wajiondoe kabisa maana watakiona cha mtema kuni.

Pia aliahidi kuhakikisha anaboresha huduma za elimu shule na afya nchini.

Alifanikiwa kuingia katika baraza la Kwanza la Mawaziri la Rais Magufuli mwaka 2016, aliwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Misimamo

Mpina amekuwa ma misimamo binafsi tofauti na wabunge wengi wa chama chake, hivyo kukumbwa na misukosuko mara kadhaa bungeni.

Katika Bunge la Bajeti Juni 23, 2012 wakati bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ya shilingi trilion 15, ikipita kwa kura 225 za ndiyo na 72 za hapana, Mpina alishikilia msimamo wake wa kuipinga na kuamua kutoka ukumbini wakati wa kuipitisha.

Aliikataa waziwazi bajeti hiyo mara baada ya kuwasilishwa bungeni na hata wakati alipochan-

Barua za Wasomaji

Dawasa hamkutenda haki

Mhariri,

Wiki iliyopita maeneo mengi ya Jiji la Dar es Salaam liliingia katika mahangaiko baada ya maji kukatika kwa siku mbili mfululizo.

Hilo lilitokana na uamuzi wa Tanesco kufanya ukarabati wa mitambo yake katika vituo vya kuzalisha maji vya Ruvu Chini na Ruvu Juu.

Inafahamika kuwa vituo hivyo ndivyo vinaipatia mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, maji kwa kiasi kikubwa.

Inashangaza kuwa viongozi wetu wanaweza kuamua kuvifunga kwa zaidi ya saa 48 vyote viwili kwa pamoja!

Hivi wakati wanafanya hivi waliwaza watu tutapata wapi maji?

Hii ni dalili kuwa ingawa viongozi hawa wape-mewa jukumu la kuwapatia wananchi maji, lakini mawazo yao wala hayawazi suala hilo.

Kama wangukuwa wanawaza kuwapatia watu maji ya uhakika, kamwe wasingefunga vituo vyote viwili kwa pamoja kwani madhara yake wanayatambua.

Ndiyo maana kwa uzembe wao, wamechulikuwa hatua na waziri mwenye dhamana.

Rose Josephat.

Mbezi, Dar es Salaam.

Stendi Mwenge ilijengwa kwa maonyesho?

Mhariri,

Inashangaza kuwa ujenzi wa stendi mpya ya daladala katika eneo la Mwenge, Dar es Salaam, ulikamilika miezi kadhaa iliyopita, lakini hadi leo stendi hiyo haitumiki.

Kuna msongamano mkubwa wa magari ya daladala yanayopakiki nje ya stendi hiyo wakati kule ndani ya stendi kupo wazi kabisa na kunaonekana kukamilika kwa kilahatua.

Wananchi wengi tunajiuliza, kwa nini stendi hiyo haitumiki wakati ilijengwa ili itatue tatizo la kutokuwepo stendi rasmi na nzuri? Au basi, tueleze kuwa kukamilika kwa stendi hiyo, ni kutimiliza kauli ya mkuu wa mkoa huo, kwamba sasa jiji lake, linakwenda kuwa kivutio kwa kila jengo linalojengwa?

Je, tuamini kuwa sasa stendi hiyo ni pambo na haikujengwa ili itumike?

Mary Joseph,

Mwenge, Dar es Salaam

Barabara ya Moro – Dom inahitaji kujengwa upya

Mhariri,

Barabara inayounganisha mikoa ya Morogoro na Dodoma, ni mbovu mno na sasa yahitaji ukarabati wa haraka ili kunusuru uhai na uharibifu wa mali.

Watumiaji wa barabara hiyo ni mashuhuda jinsi ilivyo mbovu, kwani sehemu nyingi za barabara hiyo zimejaa viraka, huku baadhi ya sehemu zikiwa na kingo zilizomeguka na kuifanya kuwa nyembamba.

Ukizingatia wingi wa magari yanayotumia barabara hii na jinsi barabara inavyozidi kuwa nyembamba, unaona kuwa kuna hatari ya ajali ambazo zinanyemelea.

Ni matarajio yangu kuwa wahusika watalichukua suala hili kwa uzito unaostahili ili kuokoa madhara yanayoweza kutokea.


Hamisi Juma


Ifakara, Morogoro.

NUKUU



Kila binadamu - “ni cha kupewa,” amepewa zawadi kuu ya uhai bure, lakini isivyokuwa bahati, watu wachache wenye uwezo mkubwa wa kiuchumi, wanakuwa wachoyo na wasiokuwa na msaada kwa wenye uhitaji. Waachwe! – Askofu Kanisa Katoliki, Jimbo la Mafinga, Vincent Mwangala wakati wa mazishi ya Mzee Cornel Mgalama (84), Kijiji cha Kinyanambo, Mafinga, Iringa – Julai 5, 2024.





Wabunge waliofukuzwa wapasua Chadema



Wabunge 19 waliofukuzwa Chadema

Na Maregesi PAUL

WABUNGE 19 wa Viti Maalum waliovuliwa uanachama na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), wameendelea kukigawa chama hicho.

Hali hiyo imedhihirika mwishoni mwa wiki, baada ya makamu mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu, kuandika ujumbe katika mitandao ya kijamii akionyesha kutoridhishwa na kampeni za chini-chini zinazofanywa na baadhi ya viongozi wenzake wanaotaka wabunge hao wasamehewe na “kurudishwa kundini.”

Akizungumza na Pambazuko, Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itifaki na Mambo ya Nje wa Chadema, John Mrema, alionekana kuwa na msimamo wa wastani akieleza uwezekano wa wabunge hao kusamehewa, lakini akasita kuzungumza kwa undani akitaka suala hilo liachwe kwa sababu liko mahakamani kwa sasa.

Wabunge hao walivuliwa uanachama Novemba 27 mwaka 2020 kwa tuhuma za kujiteua kuwa wabunge wa viti maalum wa chama hicho.

Katika ujumbe wake, Lissu alisema haoni sababu wabunge hao kusamehewa kutokana na msimamo waliyoitoa kutetea hatua yao ya kukisaliti chama ikiwamo kula kiapo mahakamani wakipinga kuvuliwa uanachama wa Chadema.

Lissu aandika

“Kama wanaruhusiwa kurudi, itakuwa ni kwa sababu hawakuwa na makosa yoyote, ila sisi ndiyo tuliwakosea. Kama tukiwaruhusu kurudi, maana yake ni kwamba, sisi wote viongozi wa chama, tulikuwa waongo, ila wao ndiyo walikuwa wakweli...”

“Kumbukeni tuliyoyasema hadharani na kwenye vikao vya chama na waliyoyasema wao hadharani na mahakamani kwa kiapo...”

“Sisi tulisema Kamati Kuu haikuwateua wao na wala haikuteua mgombea yeyote wa viti maalum na katibu mkuu wetu hakuwahi kujaza fomu za uteuzi zilizokabidhiwa kwake na Tume ya Uchaguzi kama inavyotakiwa na sheria za uchaguzi...”

“Wao walidai mahakamani kwa kiapo kwamba walikwenda kuapa ubunge kwa baraka za chama

Sumaye: Magufuli nusura azamishe...

Inatoka Uk. 17

onekana unaleta fujo, sasa tukaamua kuwa wenye viwanda wao ndio waagize sukari...”

“Kwa hiyo, wao kwa sababu wana interest (maslahi) sukari izalishwe, lakini hatutaki watu wakose sukari ile gap (pengo) tulikuwa tunahakikisha wao ndiyo wanaoagiza walikuwa wanafanya vizuri tu miaka yote hatujawahi kusikia tatizo...”

“Sasa kilichotokea mwaka huu mimi sielewi maana Waziri wa Kilimo (Hussein Bashe) anasema tumewapa waagize hawakuagiza, sasa kwani? Kwa hiyo mimi nilisikiliza ule ubishi wao bungeni, nikaona haunisaidii, lakini ukweli kuna tatizo.

“Sielewi kwanini mwenye kiwanda apewe kibali cha kuagiza sukari asiagize wakati sukari haipo na ndiyo biashara yake. Hapo kuna tatizo,” ameshangaa.

Sumaye alionyesha kushangazwa pia na hatua ya kumwadhibu Mpina bila kushughulikia tatizo lililomwingiza matatizoni.

Akifafanua, amesema hata kama Mpina alikuwa amekosea, lakini ukweli ni kuwa tatizo la sukari lipo.

“Sasa wamwemwadhibu Mpina, lakini hatujaambiwa tatizo la sukari lililoibuliwa limetatulikwa vipi,” akaongeza mhitimu huyo wa Chuo Kikuu cha Havard, Marekani na Egerton, Kenya.

Wabunge waliofukuzwa wapasua Chadema

Inatoka Uk. 20

na walimtaja katibu mkuu, kuwa alijaza fomu zao za uteuzi...

“Tulisema hadharani, kwamba walikiuka maagizo ya kamati kuu kutotambua uchaguzi mkuu na matokeo yake, huku wengi wao wakiwa wajumbe wa kamati kuu na viongozi waandamizi wa chama...”

“Wao walidai hawakufanya kosa lolote kwa mujibu wa katiba na kanuni za chama, ila dhana ya wao kuomba msamaha ina matatizo makubwa kimantiki kwa sababu baada ya kuwafukuza uanachama, walikimbilia mahakamani kwa madai kwamba tumewakosea...”

“Waliendelea kudai hivyo hata baada ya Mahakama Kuu kuamua kwamba kamati kuu haiukosea kuwafukuza na sasa wamekata rufaa dhidi ya uamuzi wa Mahakama Kuu,” ilisomeka sehemu ya andiko hilo.

Lissu anasema kuwa ni hatua mbaya sana kwa ustawi wa Chadema kuwarudisha wabunge hao aliowaita “wasaliti.”

“Kama tunataka warudi, haiwezi ikawa ni




**Makamu
Mwenyekiti
wa Chadema,
Tundu Lissu**

kwa sababu siyo wasaliti na hawakukosea, bali itakuwa ni kwa sababu hatuna tena nguvu au ujasiri wa kupambana na watu wa aina hii,” alihitimisha Lissu katika ujumbe wake huo.

Alipoulizwa zaidi kuhusu msimamo wa Chadema ni upi kwa wabunge hao ambao Lissu amewazungumzia, Mrema alisema suala la wabunge hao kurudi ama kutorudi katika chama litajadiliwa na kuamuliwa na chama kwa mujibu wa katika ya chama chao.

“Hilo andiko la Lissu nimelisoma, ila ninachosema ni kwamba hao watu wana kesi na chama chetu huko mahakamani. Kwa siyo, siwezi kuwazungumzia sana hadi hapo shauri lao litakapotolewa uamuzi na Mahakama ya Rufaa.

“Pamoja na hayo, hawajawahi kuomba msamaha tangu chama kilipowachukulia hatua, lakini ikitokea wakaomba msamaha, chama kitawajadili kupitia kamati kuu kwa sababu kanuni zetu zimeweka wazi utaratibu wa mtu aliyevuliwa uanachama anatakiwa afanye nini ili arudishiwe uanachama wake,” alisema Mrema.



Arrisallah Islamic yanuia kuimarisha elimu Morogoro

Na Mwandishi WETU, Kilosa

MKUU wa Wilaya ya Kilosa, Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, ameunga mkono juhudi za Taasisi ya Arrisallah Islamic Base kwa kuwa kinara wa kusaidia jamii yenye uhitaji.

Katika mkutano mkuu wa tatu wa mwaka wa taasisi hiyo uliofanyika juzi – Jumamosi, mjini Kilosa, Shaka aliyewakilishwa na Ofisa Tarafa wa Masanze, Malisa Ibrahim, alisisitiza umuhimu kwa jamii kuthamini kilimo, elimu, na afya kama msingi wa maendeleo ya taifa letu.

Malisa alieleza kuwa asilimia 85 ya wananchi wa Kilosa wanategemea kilimo kama chanzo cha uchumi wao, hivyo, mpango wa Arrisallah wa kuwasaidia wakulima unatarajiwa kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

Aidha, katika hotuba yake, Shaka aliwataka viongozi wa dini kukemea vitendo vya kishoga na usagaji vilivyoanza kushamiri wilayani humo.

“Bila viongozi wa dini kushikamana na seri-

kali katika kulaani vitendo hivyo, jamii itazidi kumong’onyoka kimaadili na hatimaye taifa kuwa na watu waliodumaa kifikra...”

“Viongozi wa dini naomba jitokezeni kukemea vitendo hivi kila mnapopata nafasi ya kufanya hivyo, ili kuwa na jamii inayojiheshimu na kumugopa Mungu”, alisema Shaka.

Kwa upande wake, Kaimu Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kilosa, Joha Mohamed, alisema chama hicho kinaunga mkono jitihada za Taasisi ya Arrisallah kwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan anasisitiza umuhimu kuthamini kilimo, elimu, na afya ili kuboresha maisha ya Watanzania.

Awali, Mwenyekiti wa Taasisi ya Arrisallah Islamic Base, Kassim Maringo, alieleza juhudi za taasisi hiyo kuanzisha shule ya msingi jumuishi kwa watoto wenye mahitaji maalum zimefikia hatua nzuri ingawa bado michango mbalimbali ya wadau inahitajika ili kukamilisha malengo.

Maringo alisema hatua hiyo inalenga kusaidia jamii kuepukana na unyanyapaa kwa watoto wanaozaliwa wakiwa na changamoto ambazo baadhi ya watu huamua kuwatenga, hivyo kuwa mzigo kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Taasisi ya Arrisallah Islamic Base imeendelea kuwa na mchango mkubwa kuboresha maisha ya wananchi wa Kilosa kupitia miradi mbalimbali inayolenga kuinua sekta za kilimo, elimu, na afya.



**MKUU wa
Wilaya ya
Kilosa,
Morogoro,
Shaka Hamdu
Shaka**

Je wajua



Nchi ya Uganda inajulikana pia kama 'Pearl of Africa' jina hili linatokana na vitabu vilivyoandikwa na Wiston Churchill mwaka 1907.



Nyoka ana uwezo mkubwa wa kuhisi tetemeko la Ardhi kwa umbali wa kilomita 121 (75 maili) na hata siku tano kabla ya tetemeko halijatokea.

Mnada Pugu wageuzwa...

Inatoka Uk. 15

ayotoka bila vibali umekithiri na umekuwa ukisababisha mgogoro kati ya mkuu huyo wa mnada na baadhi ya wafanyakazi wengine mnadani hapo.

Chanzo hicho cha kuamini-ka kinasema kuwa, katika tukio moja la Ijumaa ya Juni 7, mbuzi walitolewa bila vibali na baada ya mtu mmoja kuhoji, walifanikiwa kupata malipo ya mbuzi 150 ambao tayari walishachepushwa kutoka kwenye mnada huo.

"Kwa hiyo mara ya pili ikafanyika, yule mtu hakufanikiwa kuwaona wakati wanawaondoa wale mbuzi, lakini alipohoji, ndiyo changamoto zikaanzia hapo...

"Gari lilipoondoka Pugu, huyo mtu hakuiona ila katika kufuatilia, inasemekana alipiga simu kwa mhasibu wa Machinjio ya Vingunguti, ili kujiridhisha ambapo mhasibu alimweleza hakuwa eneo la kazi ila akasema kuna vijana wake ngoja awapigie.

Mzunguko wa mnada

Kuhusu mapato ya shilingi milioni 100 kwa siku 11 Byamungu alisema kamati hiyo ilifanya kazi mwezi wa 12, kuanzia Desemba 22, 2023 hadi Januari 2, 2024 ambacho ni kipindi cha msimu wa sikukuu, hivyo mauzo yanakuwa juu sana.

Byamungu alisema kwa sasa mzunguko wa mnada huo kiuchumi ni kati ya shilingi milioni 800 hadi shilingi bilioni moja kwa mwezi, kwa thamani ya mifugo inayoingia na kuuzwa katika mnada huku wakiingia watu 800 hadi 1,000 hivyo ni eneo muhimu kiuchumi.

Mtangulizi wa Ulega alinena

Machi 11, 2021 aliyekuwaziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alielekeza uongozi wa mnada huo wa Pugu, hadi kufikia Juni, mwaka 2024, uongeze mapato hadi kufikia zaidi ya shilingi bilioni 3 kwa mwaka.

Ndaki aliyasema hayo baada ya kutembelea na kuona maendeleo na changamoto zinazoukabili mnada huo.

Alisema ukusanyaji mdogo wa mapato unaotokea katika mnada huo unatokana na uzembe unaofanywa na baadhi ya viongozi wanaosimamia eneo hilo.

"Nataka tarehe 30 Juni,

makusanyo yenu yawe shilingi bilioni 3 au zaidi. Hicho ndicho ninachotaka zaidi kwenye mnada huu, hayo ndio maelekezo yangu kwenu, tufanyeni kazi kwa uadilifu, tuacheni hizi kona kona," alisema Ndaki.

Gari lilipoondoka Pugu, huyo mtu hakuiona ila katika kufuatilia, inasemekana alipiga simu kwa mhasibu wa Machinjio ya Vingunguti, ili kujiridhisha ambapo mhasibu alimweleza hakuwa eneo la kazi ila akasema kuna vijana wake ngoja awapigie.



Mtoto wa Mvuvi

Na Maregesi PAUL



Tukaboreshe taarifa Daftari la Wapiga Kura

SERIKALI kupitia Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) imetangaza kuanza kwa zoezi la kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Maboresho hayo yanayotarajia kuanza mwisihoni mwa mwezi huu – Julai, 2024, ni sehemu ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba mwakani.

Uboreshaji wa daftari hilo ndio pia ambao utazaa orodha ya watu watakaokuwa na sifa ya kuchagua viongozi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika baadaye mwaka huu.

Kwa maana hiyo, ni wakati sasa kwa kila Mtanzania mwenye sifa za kupiga kura, kuhakikisha anaboresha taarifa zake katika daftari hilo ili aweze kuwa na sifa za kuwachagua viongozi atakaoona wanafaa kuongoza.

Ni vyema kila mmoja, akaanza kumkumbusha mwenzake na kuelezana juu ya umuhimu wa zoezi hilo ambalo ndilo litakalotoa mwelekeo wa wapiga kura, na hivyo aina ya viongozi watakachaguliwa.

Watanzania tusipuuzie uboreshaji wa taarifa zetu kwenye daftari la wapiga kura, tusikae vijiwani na kujifanya hatujasikia, tusishinde mashambani tukilima na kuvuna mazao yetu, tusishinde maofisini tukifanya kazi, bali tujitokeze kwa wingi wetu katika vituo vyote vitakavyokuwa vikiboresha taarifa zetu.

Mbali na kwamba uboreshaji huo unatumia mabilioni ya fedha za walipa kodi, lakini ndio

utawapatia Watanzania haki ya kupiga kura.

Bila kuboresha taarifa, hasa zile zenye kaso-ro, kuna uwezekano wa kukosa haki ya kupiga kura kuchagua viongozi uchaguzi utakapofika.

Kila mahali, kwenye majiji, miji, mikoa, wilaya, kata, vijiji, mitaa na vitongioji, tuelezana umuhimu wa kuboresha taarifa zetu ili tupate fursa ya kupiga kura kuwachagua viongozi tunawataka.

Mliohama makazi msijisahau kwenda kwenye vituo vya kuboresha taarifa zenu, mliopoteza kadi za wapiga kura nendeni mkapate kadi mpya na wote ambao mmeshafikisha umri wa kupiga kura, nendeni kwenye vituo hivyo ili mkajandikishe.

Viongozi wa vyama vya siasa na nyinyi msikae kimya, bali waelezeni wanachama na wafuasi wenu, kwamba suala la kuboresha taarifa katika daftari ni muhimu na wananchi wote wanatakiwa kuliunga mkono.

Viongozi wa dini popote mlipo hubirini mambo ya Mungu huku mkikumbuka kuelezea taarifa za INEC, mkisema waumini wote wanatakiwa kushiriki kwenye zoezi la uboreshaji wa taarifa zao katika daftar.

Tukishafanya hayo na mengine ya msingi yanayoelezwa na tume yetu ya uchaguzi, naamini Watanzania wengi watajitokeza katika maboresho hayo ambayo ni muhimu kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu pia.





Green Horizon
Mowing & LawnCare

GO GREEN
GO CLEAN

Save 20% on your first booking with us!

OUR SERVICES

Domestic and Outside Maintenances
Garden,
Mowing and lawn care,
Pressure Washing
Tree and hedge trimming
Land scaping Design
Garden Renovation



HELPING TO KEEP OUR COMMUNITY CLEAN



0713-821 441
0672-782 223



Makongo CCM



Mowinandlawn_care



Mpina ameanza safari au anafika mwisho?



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe

Inatoka Uk. 18

gia, alisema kuwa inakinzana na Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Juhudi za mawaziri; William Lukuvi na Stephen Wassira kumshawishi mbunge huyo hazikuzaa matunda.

Hata baada ya kuitwa mara mbili akiwa nje na jina kutajwa mara mbili bila kuitikia, yeye alisema anayo mambo mengi ya kusema kuhusu bajeti hiyo aliyoikataa tangu awali na kusisitiza kuwa ataweka wazi sababu za kutopiga kura katika mkutano wake na waandishi wa habari.

Mei 2013, Mpina alitajwa kuwa miongoni mwa wabunge wa CCM waliokuwa wamejipanga kwa lengo la 'kumalizana' watakapokutana na mwenyekiti wa chama hicho tawala wakati huo, Rais Jakaya Kikwete.

Ni wakati huo ambapo kutokana na tabia yake ya kuikosoa serikali kwa kauli nzito, Mpina aliendelea kuhusishwa na wapinzani huku baadhi ya wabunge wakishinikiza aadhibiwe na

wakitaka hata avuliwe uanachama wa CCM.

Matukio tata bungeni

Hii siyo mara ya kwanza kwa Mpina kuzingirwa na kushambuliwa na wabunge wenzake kutokana na misimamo yake ambayo amekuwa akiionesha na kuisimamia wakati wote.

Mei 4, 2023, Mpina alitakiwa kuwasilisha ushahidi bungeni, baada ya kuingia katika mgogoro na Bunge, ambapo alitakiwa apeleke ushahidi wa namna gani serikali imeshindwa kutekeleza maa-gizo ya waziri mkuu.

Juni 4, 2024 Mpina aliingia kwenye mvutano mkali na Waziri wa Kilimo, Bashe kuhusu kiwango cha sukari ambacho nchi imeagiza kwa ajili kuondoa upungufu uliopo, ambapo Mpina alisema upungufu uliokuwepo ni tani 110,000 na hivyo kuishangaa wizara kuagiza tani 410,000.

Katika maelezo ya Bashe alisema kuwa sukari hiyo imeagizwa ili nchi inaposimamisha uzalishaji mwakani, kuwepo na sukari ya kutosheleza kwa miezi miwili ambayo uzalishaji utakuwa umesimama.

Mpina aliliambia Bunge kuwa Bashe alidanganya, na hivyo Spika wa Bunge, Dkt. Tulia Ackson akamtaka kuwasilisha uthibitisho kuwa waziri amedanganya Bunge, kama ambavyo kanuni zinataka.

Spika alimpa Mpina siku 10 kuwasilisha uthibitisho kwamba Bashe amelidanganya Bunge.

Hoja iliyosababisha Mpina kutakiwa kuwasilisha uthibitisho inahusu kiwango cha uagizaji wa sukari ya ziada nje ya nchi katika kipindi ambacho viwanda vinakuwa vimesimamisha uzalishaji.

Mpina amedai kwa mujibu wa sheria, uagizaji wa sukari nje ya nchi kwa ajili ya kuziba pengo, unatakiwa uwe takriban tani 150, 000 na zabuni itangazwe.

Mpina aliwasilisha ushahidi wake kama alivyotakiwa, lakini Juni 18, 2024 Spika alielekeza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kumhoji, kwa madai ya utovu wa nidha mu, akidaiwa kudharau mamlaka ya Spika na Bunge.

Inaendelea Uk. 29

Asiimwe kweli Asiimwe, tumefeli wanadamu

*Ndiyo hivyo kwa mbinguni, pia hapa duniani,
Kumpa mtu thamani, kumzidi wa mbinguni,
Mwisho ni umasikini, na maisha ya uduni,
Sasa yalia dunia, amefeli mwanadamu.*

*Mungu wetu wa mbinguni, katupa kubwa
thamani, Kwamba watoto nyumbani, tuihaki-
ki amani, Na ndivyo wanaamini, hadi wende
mautini, Sasa yalia dunia, tumefeli wanada-
mu.*

*Watoto walozaliwa, kutokea harusini,
Na wengine kuzaliwa, mapenzi ya vichakani,
Wenyewe wanaelewa, kwetu wanayo amani,
Sasa yalia dunia, tumefeli wanadamu.*

*Lakini vita vya kwetu, na tamaa duniani,
Vinatuondoa utu, na akili za vichwani, Kuyafa-
nya mambo butu, kama vile hayawani, Sasa
yalia dunia, tumefeli wanadamu.*

*Matukio ni lukuki, watoto wa msambweni,
Kama vile tuna chuki, vipi waje duniani,
Badala ya kulaiki, tunawapiga mpini,
Sasa yalia dunia, tumefeli wanadamu.*

*Tazama unyanyasaji, nyumbani na mitaani,
Mambo ya ukeketaji, unatutoa lindoni, Ya
kufanya hatuchuji, twawaweka matatani, Sasa
yalia dunia, tumefeli wanadamu.*

*Ulawiti ubakaji, sodoma ya duniani,
Unakuta wafanyaji, waheshimiwa nyumbani.
Waacha utongozaji, wafanya ya uhaini,
Sasa yalia dunia, tumefeli wanadamu.*

*Yalitokea zamani, tukadhani ya zamani,
Nje na hapa nchini, maisha kutothamini,
Tena watoto nyumbani, walinzi ni mashetani,
Sasa yalia dunia, tumefeli wanadamu.*

*Asiimwe kweli Asiimwe, asiwepo duniani,
Na hivihivi alimwe, na waliokuwa lindoni,
Mwili wake utazamwe, bila viungo mwilini,
Sasa yalia dunia, tumefeli wanadamu.*

*Likuwa wapi jamii, kuihakiki amani,
Mbona ni laana hii, sote twawa macho chini,
Jamani hatusikii, tutaja tupwa motoni?
Sasa yalia dunia, tumefeli wanadamu.*

*Waloongoza ukora, akili zimo kichwani,
Wameiharibu sura, hatunaye duniani,
Kwa hasira tunafura, ila hatuoni ndani,
Sasa yalia dunia, tumefeli wanadamu.*

*Ulinzi watoto wetu, sasa tumwachie nani?
Kama sisi sisi watu, twawatia mautini?
Tukifanye nini kitu, unyama wende shimoni?
Sasa yalia dunia, tumefeli wanadamu.*

*Jamii yetu amka, tuendako ni shimoni,
Kila mtu zamu shika, watoto iwe amani,
Haya mambo takataka, hakiki hatuyaoni,
Sasa yalia dunia, tumefeli wanadamu.*

*Kuua kwa utajiri, hiyo ni faida gani?
Mbona ni kuleta shari, duniani na mbinguni?
Hilo vema kukariri, hebu tulete amani,
Sasa yalia dunia, tumefeli wanadamu.*

*Ni vema tukumbushane, tukiwapo duniani,
Kwamba tuthaminiane, na wana wetu nyum-
bani, Tena sote tutunzane, tusiishi kishetani,
Sasa yalia dunia, tumefeli wanadamu.*

*Mtu anayejiumba, hakunaga duniani,
Ni Muumba atuumba, tuonekane mwilini,
Albino kamuumba, asiishi mashakani,
Sasa yalia dunia, tumefeli wanadamu.*

*Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)
lwagha@gmail.com 0767223602*



Mtoto Asiimwe

Uhuru wa Marekani



Askari wa Marekani wanaofanya shughuli zao ubalozi wa nchi yao Tanzania, wakishiriki kwenye sherehe za uhuru wa nchi yao zilizofanyika, Dar es Salaam.

Sherehe uhuru wa Marekani zafana Dar

Na Mwandishi WETU

KUMBUKIZI ya miaka 248 ya Uhuru wa Marekani, ilifana kwa sherehe, baada ya balozi wa nchi hiyo Tanzania, Michael Battle kualika watu wa kada mbalimbali nyumbani kwake, Dar es Salaam, Alhamisi iliyopita.

Marekani ilipata uhuru wake Julai 4, hivyo kila inapofika tarehe hiyo, nchi hiyo, na balozi zake zote, huadhimisha kukumbuka ilikotoka, ilipo na inakoelekea.

Katika kumbukizi ya mwaka huu, Marekani ililenga zaidi kuenzi urithi na uamsho mpya wa utamaduni wa Harlem (Harlem Renaissance); harakati ya utamaduni uliostawi katika miaka ya 1920 na 1930 huko Harlem, New York.

Kipindi hicho kinatajwa kuwa kilibeba taswira ya kuzaliwa upya kwa sanaa, muziki, na fasihi ya Wamarekani Weusi.

Ni katika kumbukizi ya mwaka huu, Marekani na watu wake, inasisitiza mchango wa



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, (kushoto), akisalimiana na Balozi wa Marekani nchini, Michael Battle wakati wa Sherehe ya Maadhimisho ya miaka 248 ya Uhuru wa Marekani, jijini Dares Salaam, Julai 4, 2024.

kudumu wa Harlem Renaissance kwa utamaduni wa Marekani na kuhimiza thamani ya uhuru na ubunifu - kwa wasanii, ambayo ni misingi ya utambulisho wa Marekani.

Katika maadhimisho ya uhuru wa nchi hiyo kwa mwaka huu yaliyofanyika Dar es Salaam, muziki ulitawala zaidi, huku wageni walioalikwa wakipata fursa ya kuburudika kwa muziki wa jazz, usomaji wa fasihi, na maonyesho ya sanaa mbalimbali.

Ziara ya Majaliwa Iringa

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa jana, ameendelea na ziara mkoani Iringa ambapo ameweka jiwe la msingi la ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Iramba iliyopo katika Kijiji cha Iramba, Kata ya Itandula kwenye Halmashauri ya Wilaya Mufindi. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)



Mpina ameanza safari au anafika mwisho?

Inatoka Uk. 26

Uwaziri

Akiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi katika Serikali ya Awamu ya Tano, Mpina alisimamia Oparesheni ya kutokomeza uvuvi haramu ambapo aliteketeza nyavu zinazotumika katika uvuvi haramu zilizokamatwa katika Mwanza, Kigoma na Ruvuma.

Oparesheni hiyo ililalamikiwa na ilianza kutumiwa na wanasiasa wenzake kumchafua, wakidai kuwa amekuwa chanzo cha kuwafukarisha wavuvi, kauli ambayo Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alitumia pia hivi karibuni wakati akijibu hoja za Mpina bungeni.

Akiendelea na oparesheni hiyo, Juni, 2018 Mpina alisimamia upimaji wa urefu wa samaki aina ya sato kwa kutumia rula kwenye mgahawa wa Bunge mjini Dodoma, baada ya kupata shaka kwamba wako chini ya sentimita 25 zinazoelekezwa kisheria, hatua iliyomuingiza matatani na Bunge.

Hatua hiyo ilimuibua aliyekuwa Spika wa Bunge, Job Ndugai ambaye alieleza masikitiko yake na kumlazimu Mpina kuliomba radhi Bunge kwa kitendo cha maofisa wa wizara yake kuingia kwenye mgahawa wa Bunge.



Spika wa Bunge wa zamani, Job Ndugai

Buriani



*Mwanazuoni,
Profesa Asafu
Abraham
Maradufu*

Pumzika sasa Prof Maradufu, umetimiza kazi

Na Mwandishi WETU

TANZANIA imepoteza mwanasayansi wake maarufu ambaye ametumia elimu, ujuzi na uzoefu wake kuleta mageuzi katika utafiti na hatimaye tiba na kinga za magonjwa ya binadamu.

Mwanazuoni huyo, Profesa Asafu Abraham Maradufu, sasa amelala katika Makaburi ya Njiro, Arusha. Alifariki dunia alfajiri ya Juni 30, 2024 jijini Arusha.

Pamoja na kwamba Profesa Maradufu, amelala kwenye nyumba yake ya milele, bado ataendelea kukumbukwa kwa namna ya pekee kwa kuwa alitumia usomi wake kwa manufaa makubwa na wala “siyo kunyanyua mabega,” wala kujaa kiburi cha elimu, kama wanavyofanya wengine.

Wapo wasomi wenye ngazi yake na hata kumzidi, ambao kwao, sifa kubwa ni kuwa na elimu ya juu, bila kuwa na mchango wa maana kwa taifa, achilia mbali familia yake.

Huyu Profesa Maradufu alikuwa wa tofauti sana, hakuwa mjivuni, na aliacha matokeo ya utafiti wake, ndiyo yamtambulisha na siyo wengi wa vyeti.

Prof. Maradufu ambaye aliwahi kuwa Ofisa Mtafiti Mkuu wa Taasisi ya Utafiti ya TPRI, Arusha na baadaye Uchunguzi wa Magonjwa

ya Binadamu (NIMR), Amani, Tanga.

Alimaliza masomo yake ya Shahada ya Uzamivu katika Chuo Kikuu cha McGill, kilichoko katika Jimbo la Quebec, Canada mwaka 1973, mahali ambapo alirudi kufanya Post Doctoral Research.

Shahada yake ya kwanza na ya pili alizipata kutoka katika Chuo Kikuu cha Dublin, nchini Ireland mwaka 1971.

Alikuwa ‘visiting Professor’ kwa vyuo vikuu vingi vya nchini Marekani. Alifundisha katika Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya na Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki, Baraton, kilichopo Eldoret, Kenya.

Amechapisha machapisho mengi ya kisayansi, ambayo yamekuwa rejea katika vyuo vikuu vingi vya tiba na sayansi ya afya ya binadamu.

Katika kuthibitisha usomi wake kuwa na mchango kwa taifa, Prof. Maradufu ni mmoja wa wagunduzi wa dawa ya kutibu malaria, ambayo inasifika kwa kuwa na uhakika wa asili-mia zaidi ya 82 kutibu ugonjwa huo.

Kati ya maandiko yake, lipo andiko la dini, “Creation Week, God’s Love in Action.” Andiko hilo lilichapishwa katika Jarida la Makao Makuu ya Kanisa la Wasabato Ulimwenguni (GC), Washington DC (2000), USA.

Lala salama Pro. Maradufu, hakika matendo na matokeo ya usomi wako utabaki milele.



Mtafiti wa tiba, Dkt. Askwar Hilonga (Kushoto), aki-toa faraja kwa Derek Murusuri, mwanafamilia wa Profesa Asafu Abraham Maradufu.



Uingereza haitapeleka wakimbizi Rwanda



*Waziri Mkuu wa
Uingereza, Sir Keir
Starmer*

WAZIRI Mkuu mpya wa Uingereza, Keir Starmer ameahidi kufutulia mbali mpango wenye utata wa kuwasafirisha maelfu ya waomba hifadhi kutoka Uingereza hadi Rwanda.

Katika tangazo lake la juzi, Jumamosi, kiongozi huyo mpya wa Chama cha Labour, alitangaza kuwa sasa nchi yake inasikitisha mpango huo.

Serikali iliyopita ya kihafidhina ilitangaza mpango huo kwa mara ya kwanza mwaka 2022 wa kupeleka Rwanda wahamiaji waliofika Uingereza bila kibali.

Katika mkutano wake wa kwanza na waandishi wa habari tangu kuwa waziri mkuu, Starmer alisema kuwa sera ya Rwanda itafutiliwa mbali kwa sababu ni takriban asilimia moja tu ya wanaotafuta hifadhi wangeondolewa na ingeshindwa kuwa kikwazo kwa wahamiaji zaidi.

Mpango umekufa na kusahaulika

“Mpango wa Rwanda ulikufa na kuzikwa kabla ya kuanza. Haijawahi kuwa kizuizi,” Starmer alisema na kuongeza kuwa - “Siko tayari kuen-delea na hatua ambazo hazinifanyi kushindwa kazi zangu.”

Starmer alishinda kwa kishindi kwa kishindo uchaguzi wa kiongozi wa serikali ya nchi hiyo na kuweka historia ya Uingereza kupata kiongozi kwa kura nyingi zaidi bungeni.

Ushindi huo umemfanya kuwa kiongozi mwenye nguvu zaidi wa Uingereza tangu Waziri Mkuu wa zamani Tony Blair, lakini anakabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja na

kuboresha huduma za umma, hasa afya.

Viongozi wa Afrika wamejitokeza kumpongeza waziri mkuu huyo mpya wa Uingereza.

“Kwa niaba ya serikali na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, natoa pongezi zangu za dhati kwa Sir Keir Starmer kwa ushindi wa uchaguzi wa Chama cha Labour cha Uingereza na kuwa waziri mkuu wa Uingereza,” aliandika Rais Samia Suluhu katika mtandao wa X.

Kiongozi huyo wa Tanzania amemhakikishia Starmer kwamba wataendelea kushirikiana katika Nyanja mbalimbali.

Rais Samia aliongeza kuwa anatarajia kuendelea kuwa na ushirikiano kati ya Tanzania na Uingereza katika kutatua changamoto za kimataifa na kukuza maendeleo ya kiuchumi kwa watu wa nchi mbili.

Rais wa Nigeria, Bola Tinubu alisifu “nia na ujasiri” wa Starmer katika miaka yake yote kwenye upinzani.

“Ninatarajia kuimarisha uhusiano kati ya Nigeria na Uingereza katika maeneo yenye maslahi na kuimarisha taasisi za kidemokrasia,” amesema katika taarifa yake.

Rais wa Kenya, William Ruto amesema ushindi wa Starmer ni “ushuhuda wa shauku kubwa ya raia wa Uingereza katika mabadiliko ya sera.”

Katika taarifa yake, Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini amesema anatazamia kufanya kazi na Waziri Mkuu Starmer ili kuimarisha uhusiano kati ya nchi hizo mbili.



Makala

Miradi mikubwa inavyoweza kuathiri uchumi



Bwawa la Mwl. Nyerere

Na Elizabeth HOMBO

UKWELI ni kwamba ustawi wa uchumi wa kila nchi, hujengwa kwenye “mwamba” wa kuwepo miradi mikubwa.

Ni miradi hiyo mikubwa hubeba mchango mkubwa katika ujenzi wa uchumi imara.

Lakini, pamoja na umuhimu wake huo, kwa upande wa mwingine, miradi hiyo ina maumivu hasa pale ambapo utekelezaji wake haujapangwa vyema.

Wachumi wanabainisha kuwa iwapo haitatekelezwa vyema, miradi hii inaweza kuwa na athari hasi kwa baadhi ya sekta za kiuchumi.

Deni la taifa

Moja ya maeneo ambayo yanaweza kuathiriwa na kiu ya utekeleza miradi mikubwa ya kiuchumi, ni kuongezeka kwa deni la taifa, jambo ambalo tayari limeshaanza kujionyesha nchini Tanzania.

Tangu nchi ianze kutekeleza miradi mikubwa, deni la taifa limeongezeka na kuanza kuzusha wasiwasi miongoni mwa Watanzania wengi.

Ongzeko la deni linatokana na ukweli kwamba utekelezaji wa miradi hii unahitaji kiasi kikubwa cha fedha ambacho aghalabu hupatikana kupitia mikopo.

Mwenendo wa deni la Taifa la Tanzania unaonyesha kuwa Machi, 2024 lilikuwa shilingi trilioni 91.7 ikilinganishwa na shilingi trilioni 77 katika kipindi kama hicho mwaka 2023 sawa na

ongzeko la asilimia 19.1.

Ni wazi kwamba ongezeko hilo la deni la taifa limesababishwa kwa kiasi kikubwa na deni la nje ambalo ni mikopo kwa ajili ya miradi mikubwa.

Miongoni mwa miradi mikubwa ambayo inatekelezwa kwa fedha za mikopo ni pamoja na Mradi wa Kufua Umeme wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) wenye thamani ya shilingi trilioni 6.6.

Mradi huo ni muhimu sana kiuchumi kwani utakapokamilika utakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 za umeme na kuliondoa taifa kwenye upungufu wa nishati hiyo muhimu.

Mradi mwingine ni Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) ambao ni mojawapo ya miradi mikubwa ya miundombinu inayolenga kuboresha usafiri na usafirishaji nchini.

Gharama za jumla za ujenzi wa mradi huu zinakadiriwa kuwa takribani dola bilioni 9.8, kiasi ambacho sehemu yake kubwa imepatikana kupitia mikopo.

Hata hivyo, wakati miradi hiyo inaanza kutekelezwa, aliyekuwa kiongozi wa awamu ya tano, Rais John Magufuli alisema gharama zote za mradi wa SGR zinalipwa kwa mapato ya ndani kwa asilimia 100.

Lakini mrithi wake, Rais Samia Suluhu Hassan, alieleza kuwa serikali inakopa ili kujenga miradi hiyo, kwa kuwa isingeweza kufanya hivyo kwa kutumia fedha za ndani peke yake.

Kwa mujibu wa Ripoti Kuu ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo 2021/22 iliyotolewa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), mwaka 2023, serikali ya awamu ya tano iliingizia mzigo wa kulipa ziada – kwa ongezeko la dola za Marekani milioni 742.4 (zaidi ya shilingi trilioni 1.7) kwenye ujenzi wa SGR baada ya kukubali masharti yasiyo rafiki ya mkopo kutoka Benki ya Standard Chartered.

Ripoti hiyo iliweka bayana kwamba serikali ilikopa fedha hizo bila kufanya tahmini ya kina kwa kukubali “masharti ya ajabu” ya mkopo wa kibiashara wa dola za Marekani bilioni 1.46 kutoka kwa Benki ya Standard Chartered kwa ajili ya ujenzi wa SGR.

Inaendelea Uk. 33



Daraja la Kigongo- Busisi

Miradi mikubwa inavyoweza kuathiri uchumi

Inatoka Uk. 32

Mkopo huo ulitolewa mwaka 2020

Mradi mwingine ni wa Daraja la Kigongo-Busisi, Mwanza ambao kwa mujibu wa taarifa ya Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), iliyo tolewa kwa umma Aprili 22, 2024 utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 87.

Daraja hilo lenye urefu wa kilomita tatu na upana mita 28.45 na barabara unganishi zenye urefu wa kilomita 1.66, unajengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 716.333 ambazo ni fedha za serikali kwa asilimia 100.

Kuathiri bajeti za sekta nyingine

Kutumia fedha nyingi kwenye miradi mikubwa mara nyingi huilazimisha serikali kupunguza rasilimali zinazohitajika katika sekta nyingine muhimu kama vile elimu, afya, na kilimo.

Sehemu kubwa ya miradi mikubwa ipo chini ya Wizara ya Ujenzi ambayo katika mwaka huu wa fedha imetengewa shilingi trilioni 1.77.

Wizara nyingine ambayo miradi mikubwa inaangukia kwake ni Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) ambayo imetengewa shilingi trilioni 10.1 katika bajeti, likiwa ni ongezeko la takribani shilingi bilioni 981 ukilinganisha na bajeti ya 2023/24.

Ingawa kwa umuhimu wake, wizara hiyo imetengewa bajeti hiyo wizara nyingine nyeti zimeathirika.

Mathalan, bajeti ya Wizara ya Maji imepungua, hali ambayo inaweza kusababisha changamoto katika upatikanaji wa huduma za maji safi na salama kwa wananchi katika maeneo mbalimbali.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi nayo imepata upungufu wa fedha kwa asilimia ndogo ikilinganishwa na mwaka wa fedha wa 2023/24, ikimaanisha kuwa fedha nyingi zimeelekezwa kwenye miradi mingine muhimu.

Kwa upande mwingine, bajeti ya Wizara ya Kilimo imepungua, licha ya kuwa ni muhimu zaidi kwa ustawi wa wananchi.

Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara nayo imepungua, na hii inaweza kuathiri mipango ya kukuza viwanda na biashara, ambayo ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa nchi.

Wengi walitarajia kuwa wizara kama Tamisemi ambayo imepata fedha nyingi kwenye bajeti, fedha hizo zingeelekezwa kwenye miradi muhimu kiuchumi, lakini kwa mshangao bajeti ya ununuzi wa magari ndani ya Tamisemi imeongezeka kutoka shilingi bilioni 500 hadi shilingi bilioni 800.4 katika mwaka huu wa fedha.

Ukosefu wa usawa wa maendeleo

Miradi mikubwa mara nyingi hufanyika kati ka maeneo maalum na hivyo kusababisha ukosefu wa usawa kwa maendeleo kati ya miji mikubwa na maeneo ya vijijini.

Hali hii inaweza kuongeza pengo la kiuchumi na kijamii kati ya maeneo haya, hivyo kusababisha ukosefu wa usawa wa fursa na huduma.

Mfano Daraja la Tanzanite limejengwa ili kupunguza msongamano Dar es Salaam, ambako huko kuna barabara nyingi za lami, wakati kuna maeneo mengine nchini kuna shida kubwa ya barabara, vivuko na madaraja.

Athari kwa mazingira

Ujenzi wa miradi mikubwa kama vile mabwawa ya umeme na migodi, inaweza kuharibu mazingira.

Ukataji wa miti, uhamishaji wa wanyama na uchafuzi wa maji ni baadhi ya athari za mazingira zinazoweza kutokea.

Athari hizi siyo tu kwamba zinaharibu urithi wa asili, bali pia zinaweza kuathiri sekta nyingine kama vile kilimo na utalii, na hivyo kudhoofisha vyanzo vya mapato vya nchi.



Chris Brown akoleza moto bifu la Kendrick, Drake

New York, Marekani

MWIMBAJI wa muziki wa pop, Chris Brown amekoleza moto kwenye bifu la mastaa wawili; Drake na Kendrick baada ya kuonekana akiimba wimbo wa Kendrick Lamar - wa 'Not Like Us' wakati akiwa kwenye moja ya kambi za starehe katika Jiji la New York.

Pia Breezy ameibua maswali kwenye vichwa vya wengi kwani alionekana kuwa karibu na Drake na hata kwenye wimbo wa 'Family Matters,' Drake alionekana akimpa shavu.

Komasava ya Diamond yazidi kupasua anga

Paris, Ufaransa

MSANII wa bon-go flewa kutoka Tanzania, Nasib Abdul, almaarufu - 'Diamond Platnumz' amezidi kupeperusha bendera ya nchi kupitia ngoma yake ya Komasava na kuzidi kuwakosha nyota wakubwa wa fani hiyo duniani.

Hadi sasa kibao hicho 'kimeshakuna' mastaa wakubwa duniani wakiwamo Chris Brown, Paul Pogba, Destiny Udogie.

Kwa nyakati tofauti, wakongwe hao wa burudani duniani, wameonekana wakijirekodi wakati wanacheza wimbo huo na kuweka kwenye akaunti

zao za Tiktok.

Juzi wakati wa mechi ya Ufaransa dhidi ya Ureno, msanii huyo alionekana akiwa 'anakula bata' na kiungo mstaafu wa Juventus na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba.

Mechi hiyo ilimalizika kwa Ufaransa kusonga mbele kwenye hatua ya nusu fainali kwa mikwaju ya penati.

Sasa habari kubwa ni ngoma hiyo wiki hii imetumika kwenye hafla ya Washiriki wa Shirikisho la Askari wa Kike Ukanda wa Afrika (IAWP - Africa Chapter) wakati wakijiachia na ngoma hiyo katika hafla iliyofanyika jijini Abuja, Nigeria.

Rema arudi kivingine, Kiswahili ndani!

Lagos, Nigeria

MSANII wa Nigeria ambaye anafanya vizuri kwa sasa kwenye anga za muziki, Rema ametumia lugha ya Kiswahili katika wimbo wake mpya, na kuvutia mashabiki wengi hususan wanaotoka Afrika Mashariki.

Wimbo huo umepokelewa vyema na hata wasiokizungumza Kiswahili kwani wananogeshwa zaidi na "utamu" kwenye kazi hiyo mpya iliyotoka soko la muziki kwa kasi.

Baadhi ya mashairi ya Kiswahili aliyotumia kwenye ngoma hiyo ni "Ni nani hatari, ni nani mnoma sana?" "Ni wewe, Ni nani anabamba, ni nani mkali sana?", Ni nani anatamba, nani anavuma sana?", Ni nani ndo bingwa? ni wewe."



Magoli ya jioni yalivyoua Ujerumani

Na Mwandishi WETU

UKIWAULIZA Wajerumani kuhusu sababu za kuondolewa kwa timu yao kwenye michuano ya Euro 2024, watabebesha lawama kwa kila mhusika wa timu hiyo.

Watafanya hivyo kwa kuwa wachezaji, kwamba walikuwa wazembe, kwamba mwamuzi alipendelea wapinzani wao na zaidi sana, kwamba kocha hakujipanga vyema.

Lawama zote hizo zinafuatia kutolewa kwa Ujerumani kwenye mashindano hayo makubwa ya soka kufuatia kipigo cha magoli 2-1 dhidi ya Hispania.

Ujerumani iliuawa kwa goli la jioni lililofungwa na Florian Mikel Morino katika dakika ya 119, dakika moja kabla mchezo huo haujamalizika.

Awali Ujerumani nayo ilinufaika na goli la jioni kwani ilipata bao la kusawazisha katika dakika za jioni – dakika ya 89 baada ya Florian Wirtz kuzifumana nyavu na kufanya matokeo kuwa 1-1 hadi mwisho wa mchezo.

Mapema katika kipindi cha pili, La Roja aliipatia Hispania goli la kuongoza na wakati mchezo unakaribia kumalizika, watu wengi waliamini kuwa Hispania inaelekea nusu fainali, Wirtz ali-

kuwa na mawazo mengine na kusawazisha katika dakika hizo za jioni.

Hapo alifufua matumaini ya Ujerumani kupindua meza.

Lakini mambo yaligeuka tena dakika za jioni za muda wa nyongeza na kuondoa kabisa matumaini ya Ujerumani kulinyakua kombe hilo kati-ka ardhi ya nyumbani.

Matokeo hayo yamewaumiza sana wajerumani waliokuwa na matarajio makubwa ya kulibeba kombe hilo mwaka huu.

Kocha wa kikosi hicho, Julian Nagelsmann, naye alilaumu waamuzi kwa kuinyima timu yake penati ambayo ingeweza kubadili matokeo.

Tukio hilo lilitokea katika muda wa nyongeza wakati shuti lililopigwa na Jamal Musiala lilipogonga mkono wa beki wa Hispania, Marc Cucurella, aliyekuwa ndani ya eneo la hatari.

Wachezaji wa Ujerumani na mashabiki walishangilia baada ya tukio hilo wakiamini kuwa watapewa penati, lakini refa Anthony Taylor, hakuona kama lilikuwa tukio la penati.

Uamuzi wake huo uliungwa mkono na Refa Msaidizi anayetumia video (VAR).

Muda mfupi baadaye, Merino aliruka na kupiga kichwa kilichoenda moja kwa moja wavuni na kuiandikia Hispania goli la pili.

MICHEZO

Jumatatu, Julai 8-14, 2024



Kocha wa Simba SC, Fadlu Davids

Simba

wavumiliane wakati wanajenga timu

Na Mwandishi WETU

WANACHAMA na mshabiki wa Klabu ya Simba wanapaswa kuwa watulivu msimu wa ligi utaka-poanza, ili kutoa fursa nzuri kwa ujenzi wa timu yao ambayo kimsingi ni kama mpya.

Wakati timu zote zipo katika harakati za usajili, Simba imeonekana kuwa 'busy' zaidi kwenye dirisha la sasa la usajili.

Baada ya kutangaza kuachana na wachezaji wengi wa zamani, Simba inahitaji kusajili wachezaji wapya wengi ili kuziba nafasi zilizoachwa.

Tayari timu hiyo imetangaza wachezaji kadhaa; wa ndani na wa nje, ambao imewasajili na inahusishwa pia na usajili wa wachezaji wengine zaidi.

Kwa jinsi hali inavyojionyesha, timu hiyo ni kama vile itakuwa mpya msimu utakapoanza, kwani ina 'maingizo' mapya mengi na hapo ndipo suala la uvumilivu linapopewa kipaumbele.

Kwa kawaida, mashabiki wengi wa soka nchini hawana utamaduni wa kutoa muda wa kutoa kwa viongozi, makocha na wachezaji, jambo ambalo linaweza kuathiri Simba iwapo watataka

matokeo ya haraka na mazuri kwenye timu hiyo mpya.

Tayari Simba imemtambulisha kocha mpya, Fadluragman Davids, ambaye amekuja na wasaidizi wake wote na anatarajiwa kuanza kazi wiki hii akiwa na kundi la wachezaji ambao ni wapya kwake.

Katika hali kama hiyo, watalaamu wa soka wanasema kocha huyo na wasaidizi wake watahitaji muda wa kutosha kusoma wachezaji ili kufahamu umahiri na udhaifu wao, kabla hawajaanza kutekeleza mipango yao ya jinsi ya kuwatumia.

Lakini, siyo Simba peke yake ambayo ipo kwenye hali hiyo, kwani ingawa timu nyingine hazina maingizo mengi ya wachezaji wapya, lakini zimesajili watu kwenye maeneo muhimu na ili umahiri wao uonekane, watahitaji muda wa kuzoeana na waliowakuta.

Harakati hizo za usajili zimeifanya ligi ya NBC ambayo hivi sasa ipo kwenye mapumziko, ionekana kuwa bado inaendelea kutokana na mchuano wa vilabu kuwania wachezaji.

Ni mchuano mkali kuliko hekaheka tunazoziona viwanjani wakati ligi hiyo ikiendelea.

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

